**Mbappe afikiria mkataba mpya PSG**




UKURASA 21

**Harmonize kwa hili Mungu atakubariki**

UKURASA 20



**MAISHA** Nipashe Jumapili — Baba, Mama na Mwana
JANUARI 24, 2021



Mwisho wa urafiki na mwanao huanzia hapa...



MAISHA NI NYUMBA
Umuhimu wa umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba

Ukurasa 15



KIPAIMARA

Ukurasa 12


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 24, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580470

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UWEKAJI 'WEAVING'
**Urembo unaosumbua wengi**

Ukurasa 14

# Kijana adaiwa kujinyonga kisa deni la benki

UKURASA 2





Askari wa Bunge wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Martha Umbula, baada ya kuwasili katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuagwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mo Dewji kuajiri 100,000, ang'ara Afrika

UKURASA 4



## Spika ataja mauaji Kiteto mwili wa mbunge ukiagwa

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **SIMBA YASHUSHA KOCHA MKUFUNZI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Adaiwa kujinyonga kisa deni la benki

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WATU sita wamefariki dunia katika matukio tofauti mkoani Morogoro, yakiwamo ya kufa maji na kudaiwa kujinyonga huku mtu mmoja akinusurika kupoteza maisha baada ya kudaiwa kujaribu kujiua kwa kunywa sumu ya kuhifadhia mahindi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa, tukio la kwanza lilitokea Januari 13 majira ya saa 10 jioni kijijini Mmgeta wilayani Kilombero, linamhusu kijana Felisian Mwampinzi (22).

Mkulima huyo na mkazi wa Mngeta, alikutwa akiwa amefariki dunia akidaiwa kujinyonga ndani ya chumba chake kwa kutumia nguo ya kitenge huku chanzo cha kuchukua uamuzi huo kutokana na ujumbe unaodaiwa aliuacha, kwamba ameamua kujinyonga kwa kuwa anadaiwa na benki.

Kamanda Muslimu alisema katika ujumbe huo, marehemu alidai alikopa deni kwa ajili ya mama yake lakini mama yake amekataa kulilipa, hivyo anasumbuliwa na benki na ndiyo sababu ya kuamua kujinyonga ili asisumbuliwe tena.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema wakati kijana huyo anajinyonga, hakukuwa na mtu yeyote nyumbani na mwili wake ulihifanyiwa kwa ajili ya uchunguzi na baadaye ukakabidhiwa kwa ndugu zake kuendelea na taratibu za maziko.

Katika tukio la pili, Jafary Isaka (28), mkulima na mkazi wa Kijiji cha Mkula B, amekutwa akiwa amefariki dunia baada kudaiwa kujinyonga kwa kutumia kamba aliyoitengeneza kwa kuchana shuka na kuifunga kwenye moja ya kenchi ndani ya chumba chake.

Kamanda Musilimu alisema tukio hilo lilitokea mnamo Januari 16 majira ya saa 10 jioni katika maeneo ya Mkula B, Kata ya Mkula, wilayani Kilombero ambapo chanzo cha tukio hilo bado hakijafahamika kwa kuwa hakuna ujumbe wowote ulioachwa na kijana huyo.

Alisema mwili wa kijana huyo umefanyiwa uchunguzi na daktari na kukabidhiwa kwa ndugu kwa taratibu za mazishi.

Katika tukio la tatu, Cecilia Ching'unyau (22), mkulima na mkazi wa Magoweko, Tarafa na Wilaya ya Gairo, amenusurika kufa baada ya kudaiwa kujaribu kujiua kwa kunywa sumu ya kuhifadhia mahindi.

Kamanda Musilimu alisema tukio hilo lilitokea Januari 14, mwaka huu majira ya saa moja usiku katika Mtaa wa Magoweko ambapo mtuhumiwa anadaiwa kunywa sumu ya kuhifadhia mahindi aina ya Acteric kwa kuchanganya na pombe aina ya vodka-cuca.

Alisema alikutwa akiwa amelewa na kupoteza kumbukumbu huku akiwa ameegemea ukuta wa nyumba na pembeni yake kulikutwa makopo mawili vya pombe hiyo yakiwa yameshatumika na makopo mawili vyenye sumu hiyo.

Alisema mtuhumiwa amelazwa Kituo cha Afya Gairo akiendelea na matibabu na hali yake inaendelea vizuri, akidai kuwa chanzo cha tukio ni wivu wa kimapenzi kuwa wazazi wanaingilia kuvunja uhusiano na mpenzi wake.

Katika tukio la nne lililotokea Kijiji cha Mbasa, Tarafa ya Ifakara, Kilombero, mwili wa Msham Abdalah (21), mkulima na mkazi wa Kapolo, uliokotwa ukielea katika Mto Kikwawila.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issa, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, moja ya vifaa vinavyotumika kufungua magari, baada ya kuwakamata watu watano kwa tuhuma za kuhusika na wizi wa magari saba yaliyokamatwa katika mikoa mbalimbali nchini. **PICHA: ELIZABETH JOHN**.

# Watano mbaroni tuhuma wizi magari

**Na Elizabeth John,Njombe.**

WATU watano wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Njombe kwa tuhuma za kuhusika na wizi wa magari saba yaliyokamatwa katika mikoa mbalimbali nchini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa magari hayo yamekamatwa yakihusishwa na wizi baada ya msako wa kutafuta gari moja lililoibwa maeneo ya Chaugingi mjini Njombe.

Alisema magari yaliyokamatwa ni aina ya Noah linalodaiwa kuibwa mkoani Mbeya, gari aina ya Spacio lililotoka Silali mkoani Mara, Rav 4 lililokamatwa mkoani Singida na Carina lililopatikana mjini Njombe.

"Tulikuwa tunatafuta gari moja, matokeo yake tumeweza kukamata magari mengine saba ambayo yanahusishwa na kuibwa maeneo mbalimbali katika nchi yetu," alisema Kamanda Issa.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Edrick Husein, maarufu Kimyakimya kutoka Dar es Salaam, Sudy Mwinyi, mkazi wa Uyole, Mbeya, Method Mkongwa, mkazi wa Njombe, Imani Fidelis, mkazi wa Moshi na Timothy Nehemia, mkazi wa Mufindi mkoani Iringa.

Kamanda Issa alisema watuhumiwa hao wanadaiwa wanashirikiana kuiba magari na kuyapokea kisha wanayabadilisha namba na hutumia vifaa maalum katika kubadilisha namba za injini.

"Vifaa vyenyewe ukiviangalia vimeandikwa namba kuanzia 0-9, namba ambazo zipo kwenye magari ,hivi huwa vinagongwa kwenye namba endapo ukitaka kubadilisha kwenye injini au kwenye chesesi na bado kuna dawa wanayotumia kufuta namba kwa kusugua," alisema Issah.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakitumia vifaa mbalimbali katika wizi wa magari na kuyabadilisha ili wahusika wa magari hayo washindwe kuyatambua pindi wayaonapo.

Alisema watuhumiwa hao wanaonekana kuwa wazoefu, waliokuwa na mtandao kutoka mikoa mbalimbali ambao umenaswa mkoani Njombe.

Aliwataka wananchi ambao wameibiwa magari za aina hiyo, kwenda kuyatambua akionya kuwa yaliyoingizwa nchini bila kulipiwa kodi, ni lazima yalipiwe.

"Tutashirikiana na TRA ili kuhakikisha kodi ya serikali inakusanywa, haya magari yalikuwa yanamilikiwa na watu, hivyo kaa mkao wa kujibu gari namna ulivyolipata, ukieleza tofauti utakuwa sehemu ya tukio la wizi," alionya.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Njombe, Shaban Musibu, alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mpaka sasa magari saba yamekamatwa, hivyo kwa mujibu wa sheria, wamegundua kuna magari kadhaa yameingizwa bila ya utaratibu wa sheria, hivyo wahusika wamekwepa kodi.

Alisema mpaka sasa magari mawili wamiliki wake wamekwepa kodi lakini bado uchunguzi unafanyika ili kubaini kama kuna magari mengine.

"Nitoe wito kwa wanaofanya hii kazi waache kwa sababu utanunua gari ambalo limeingia kwa wizi, utakamatwa mwisho wa siku utapoteza hela," alisema Musibu.

# Mbinu kumaliza uhaba mafuta ya kula zatajwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali kupitia Wizara ya Kilimo ina mpango wa kuongeza nguvu katika uzalishaji wa alizeti ili kuhakikisha kuna mafuta ya kula ya kutosha yanayozalishwa nchini na hivyo kupunguza utegemezi wa mafuta hayo kutoka nje.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo sasa, uzalishaji wa ndani unakidhi asilimia 43 na hivyo nchi inazalisha tani 270,000 za mafuta ya kula kila mwaka na huagiza nyingine tani 600,000 kufidia pengo lililopo ndani.

Prof. Mkenda aliyasema juzi alipozuru kwenye kiwanda cha kusindika mafuta ya kula ya alizeti cha Pyxus Agriculture Tanzania cha jijini Dodoma.

Alisema pamoja na kuongeza nguvu kuhakikisha mafuta ya kula yanapatikana nchini kwa kiasi kinachotakiwa, serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwawezesha wawekezaji na pia wakulima wadogo kwa kuwapa nafasi ya kusafirisha bidhaa zao nje.

Prof. Mkenda alisema kwamba anafahamu kuna mambo kadha wa kadha ambayo yanasababishwa na kukwama kwa uzalishaji mkubwa wa mafuta nchini, hivyo serikali itapitia upya sheria na kanuni ili kuondoa mkwamo na kuwezesha uzalishaji wa ndani kukua zaidi.

Waziri Mkenda alisisitiza kuwa hakuna mageuzi ya kiuchumi yanayoweza kutokea bila kuwa na mapinduzi kwenye kilimo.

"Tukiongeza tija kwenye kilimo, bei za bidhaa kama chakula itapungua, mageuzi kwenye kilimo yatasaidia sana kukuza viwanda hapa nchini," alisema Prof. Mkenda.

Waziri huyo alisema serikali itahakikisha mbegu za kutosha za alizeti zinapatikana, akiagiza kuangaliwa kwa mfumo wa kilimo cha mkataba kwa kuboresha mfumo wake.

"Tabia ya watu kuingia mkataba lakini wakati wa kuvuna wanampa mtu mwingine haipendezi, lazima wakulima waheshimu mikataba." alionya Prof. Mkenda.

Waziri huyo aliongeza kuwa ataitisha mkutano wa wataalamu ili kuangalia upya sera na taratibu zinazotumika katika uzalishaji wa alizeti nchini.

## HABARI KITAIFA

# Spika ataja mauaji Kiteto mwili mbunge ukiagwa

**Na Augusta Njoji,DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameongoza wabunge kuaga mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Umbulla (66), huku akikumbuka namna walivyoshirikiana naye kudhibiti mauaji ya wakulima na wafugaji katika wilaya za Kongwa na Kiteto.

Wakati wa mgogoro huo, Umbulla alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, jambo ambalo Spika Ndugai alisema lilimumiza siku zote kutokana na vifo vilivyotokea.

Akitoa salamu za rambirambi, Spika Ndugai alisema: "Kiteto ni moja ya wilaya ngumu sana kiutawala, mimi ni jirani yao. Nikiwa Mbunge wa Kongwa, hakuna kitu ambacho nimelia mara kwa mara bungeni kuhusu Kiteto."

Alisema Wilaya ya Kiteto ni ngumu na kipindi Umbulla akiwa Mkuu wa Wilaya, yalijitokeza mauaji kadhaa kati ya wakulima na wafugaji.

"Tulizika mara kadhaa, kumekuwa na mapumziko miaka mitano iliyopita baada ya Rais John Magufuli kuingia madarakani, lakini sasa matatizo yameanza tena. "Hata jana (Juzi) jimboni kwangu Kijiji cha Makawa tulimzika kijana mmoja ambaye ameacha watoto wadogo sana na ameuawa kikatili.

"Kuna wakati Martha alikuwa akija ofisini kwangu, alikuwa anasema 'Job bado unakumbuka yale mambo tu', nilikuwa namjibu kuwa 'wewe mbona huhusiki?', anarudia tena ninamwambia Martha kuwa na amani, wale ndugu zetu waliuawa na matatizo yalishaisha.

"Kiteto kuna shida, tusidharau, serikali tutafute ufumbuzi wa kudumu, tusiende juu juu, tukienda juu juu kwa upande wa viongozi, hatutapata ufumbuzi, ipo shida kubwa Kiteto, ninatumai serikali yetu itaangalia Kiteto, nimewahi kusema wakati huo ilikuwa kama Somalia.

"Marehemu alijishughulisha sana na masuala ya ushauri kwenye kilimo kwa wanawake, na hapa bungeni alipendelea kuwapo kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji," alisema.

Spika Ndugai alisema Umbulla alijitoa zaidi kwenye eneo hilo na kumshukuru kwa ushauri na michango aliyoitoa kipindi cha ubunge wake.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, alisema Umbulla amechangia kuimarisha heshima na usawa wa binadamu hasa wanawake.

Awali, akisoma wasifu wa marehemu, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, alisema Umbulla ameacha mume, watoto wawili na wajukuu watatu.




Daktari wa upasuaji wa macho, Zainul Humbaro (kushoto), akimpima mgonjwa Mwachumu Twarati mkazi wa Mafia, baada ya kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho, katika kituo cha afya Medwell, kilichopo Kibaha Mpakani, mkoani Pwani jana. Huduma hiyo ya upimaji na upasuaji wa mtoto wa jicho, hutolewa bure kituoni hapo kila siku ya Jumanne na Ijumaa. **PICHA: MARGARET MALISA**

# Wasioendeleza mashamba ya ngano kunyang'anywa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Kilimo, imeingia makubaliano na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuhusu uendelezaji wa zao la ngano, huku ikisisitiza kuwanyang'anya mashamba ya ngano wale wote walioshindwa kuyaendeleza.

Miongoni mwa makubaliano hayo ni kununua kwa bei isiyopungua Sh. 800 kwa kilo moja ya ngano.

Akizungumza jana katika mkutano wa wadau wa tasnia ya ngano jijini hapa, Waziri Prof. Adolf Mkenda, alisema kilimo cha ngano na shahiri kinasuasua nchini.

"Tukiangalia zao la ngano Tanzania linadorora, uzalishaji unakwenda chini, nimepita Siha kule wanaozalisha ni wachache.

Basuto Hanang' tumekuta hata tuliyempa shamba letu, hazalishi ngano, amekamata shamba la serikali, lakini hazalishi. Kuna mashine tuliagiza kutoka Canada, ninadhani zipo kwenye maboksi," alisema.

Prof. Mkenda alisema wale wenye mashamba ya serikali, wachague kusuka au kunyoa, akimaanisha kulima ngano au kuyarudisha mashamba serikalini.

"Wale wenye mashamba ya serikali, ni kusuka au kunyoa, walime ngano au tunayachukua, wale wenye mashamba ya ngano au shahiri, wachague kulima ngano au shairi au serikali kuyachukua, hatupendi mgogoro na wawekezaji," alionya.

Alitoa wito kwa wawekezaji wote kuwekeza katika kilimo hicho ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya ndani huku akiwataka wakulima kuzalisha ngano bora yenye tija, ili kutoumiza wawekezaji.

Waziri huyo alisema kama ikiachwa hali iliyopo, inahatarisha na huenda ikaua kilimo hicho na kuwashukuru wawekezaji kwa kuanzisha viwanda vya kutumia ngano ya ndani.

"Hili zao tunalipoteza kwa kuwa ukiwauliza wakulima, wanasema tatizo ni bei, kulima kwa bei tunayoiona ni hasara hivyo wanaona walime viazi, maharage na mazao mengine, mashamba mengine ni makubwa vipande, vinakodishwa kwa wakulima na hawataki kulima ngano," alisema. Waziri huyo alisema bei imekuwa ni tatizo na kusababisha wakulima kukata tamaa kulima zao hilo.

"Rais John Magufuli alipokuwa akizindua Bunge, alitoa maagizo mengi ikiwamo kufufua zao la ngano, Tanzania tujitegemee katika zao la ngano na akasema atakayemteua kuwa Waziri wa Kilimo, kazi yake ya kwanza iwe ni kushughulikia ngano, leo siyo siku ya kwanza kwa harakati hizi," alisema.

Alisema Tanzania inaagiza ngano nje ya nchi kwa wastani wa tani 800,000 hadi milioni moja huku uzalishaji wa ndani ni kati ya tani 60,000 hadi 70,000 kwa mwaka.

"Uwezo wetu ni mkubwa kuliko tunavyozalisha, lakini tumekuwa tukicheza kati ya tani 60,000 hadi 70,000, wataalamu wanatuambia ukiangalia hali ya nchi, Tanzania ina uwezo mkubwa kuliko nchi yoyote Afrika Mashariki," alisema.

Waziri huyo alisema katika uzalishaji wa ngano, kwa sasa Tanzania ni ya pili kwa nchi za Afrika Mashariki na kwamba fursa iliyopo bado haijatumika ipasavyo.

Alisema Tanzania imeweka mikakati ya kukuza zao hilo ili kurudi kwenye makubaliano ya kutoza ushuru wa asilimia 35 kwa ngano kutoka nje.

Akizungumza kuhusu makubaliano hayo, Prof. Mkenda alisema wale wote wanaonunua ngano kutoka nje ya nchi, watanunua kwa uwiano sawa kulingana na uzalishaji wake.

"Kama unaingiza asilimia 60 ya ngano kutoka nje, utanunua asilimia 60 ya ngano inayozalishwa ndani, haya ni makubaliano kama anaagiza asilimia 10, atanunua asilimia 10 kulingana na uzalishaji, bei ya chini itakuwa ni Sh. 800 kwa kilo, wakulima wanajua, na hapa sekta binafsi wamekubali maumivu kidogo lakini wanataka ubora.

"Tunaahidi kuwa tunakaa na wadau wote kukaa kikao kila mwaka kujadili kero zote, na itafanyika kwa mazao yote ya kimkakati, tutaanzisha dawati la sekta binafsi na tutaweka mtu makini maana kuna kero zingine zinakera," alisema.

# TANESCO yapewa miezi sita umeme vijiji vyote

**Na Zuena Msuya, DODOMA**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme (TANESCO) mkoani Dodoma kuhakikisha ndani ya miezi sita vijiji vyote ya mkoa huo viwe vimepata umeme.

Dk. Kalemani alisema hayo juzi wakati wa mkutano wake na wafanyakazi wa TANESCO wa Mkoa wa Dodoma, uliokuwa na lengo la kufahamiana, kusikiliza kero zinazowakabili na kutoa maelekezo ya kuboresha utendaji kazi wa shirika hilo.

Alisema wafanyakazi hao ndiyo wenye dhamana na jukumu kubwa la kuhakikisha Mkoa wa Dodoma unapata umeme wa kutosha na wa uhakika katika maeneo yote.

Dk. Kalemani alisisitiza mkoa huo kwa sasa una wakazi wengi na bado wanaendelea kuongezeka kwa kuwa ni makao makuu ya nchi, hivyo umeme mwingi unahitajika katika shughuli mbalimbali.

Alisema kuwa kutambua hilo, ni lazima kila mfanyakazi awe sehemu ya shirika hilo na afanye kazi kwa kasi zaidi, ubunifu mkubwa na kwa usahihi ili kukidhi mahitaji ya umeme na kuboresha zaidi huduma zitolewazo na shirika hilo.

"Sitakubali kupata aibu ya baadhi ya maeneo na vijiji vya makao makuu ya nchi kutokuwa na umeme, mkoa huu una zaidi ya Megawati 400 za umeme, lakini matumizi ni Megawati 45 tu kwa sasa, kuna wateja wengi ambao wanahitaji umeme na maeneo mengine bado hayajafikiwa kabisa na huduma hiyo, TANESCO  Dodoma fanyeni kazi," aliagiza.

Alitoa siku 14 kwa shirika hilo mkoani hapa kumfikishia taarifa ya namna walivyojipanga katika kusambaza umeme kwa wananchi, kuunganisha wateja wa zamani na kupata wapya, kuzalisha na kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

Vilevile, alipiga marufuku watumishi wenye tabia ya kuchelewesha majalada ya kazi, akisisitiza kuwa vitendo hivyo vinachelewesha utendaji kazi na kutotimiza malengo kwa wakati.

"Ni mwiko na marufuku kukaa na jalada mezani zaidi ya siku moja ofisini, kama huwezi kulifanyia kazi, sema au peleka kwa wanaoweza kulifanyia kazi, tunataka kazi ziende haraka na kwa wakati, ukiona huwezi kufanya kazi kwa kasi hii ninayotaka, ni bora uondoke ofisini," alionya.

Katika hatua nyingine, Dkt. Kalemani aliiagiza TANESCO, kuangalia upya utaratibu wa kuajiri au kuwapa kazi wafanyakazi wa muda maalum (STE) ambao muda mwingi wanakuwapo maeneo kazi kufanya kazi za kuchimba mashimo, kusimika nguzo na kuvuta nyaya.

Alitaka STE wasiokuwa na mikataba, wapewe mikataba, wenye sifa ya ajira waajiriwe na wale wasiokuwa na sifa na wamefanya kazi muda mrefu, wapewe mafunzo maalum ili wapate ajira.

# Mo Dewji azidi kung'ara orodha mabilionea Afrika

## ■Mwenyewe kutoa ajira 100,000

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA Mohammed Dewji, maarufu Mo, ameendelea kung'ara kwenye chati ya mabilionea wa Afrika, mwaka huu akiorodheshwa namba 13 katika ripoti ya Jarida la Forbes, 2021.

Katika ripoti hiyo Mo (45) amepanda kutoka nafasi ya 16 mwaka jana akiwa na utajiri wa Dola za Marekani bilioni 1.6, na ameendelea kuwa bilionea kijana zaidi katika orodha hiyo ya mabilioni 18 barani kwa miaka sita mfululizo.

Ripoti hiyo iliyotoka juzi, inabainisha kwamba, mfanyabiashara tajiri kutoka Nigeria, Aliko Dangote (63), ameendelea kuwa kinara kwa mara ya 10 mfululizo, akiwa mtu tajiri zaidi barani Afrika.

Dangote anayejihusisha na biashara ya saruji, sukari na unga wa ngano, ana utajiri wa Dola za Marekani bilioni 12.1.

Nafasi ya pili imeendelea kushikiliwa na rais wa Misri mwenye umri wa miaka 60, Nassef Sawiris mwenye utajiriwa Dola bilioni 8.5, akifuatwa na Nicky Oppenheimer (75) wa Afrika Kusini mwenye utajiwa wa Dola bilioni nane.

KAULI YA MO

Baada ya kutolewa kwa ripoti hiyo, Mo Dewji alisema jana kuwa kwa sasa ameajiri watu 33,000 na anatarajia kutoa ajira kwa watu 100,000 katika miaka minne ijayo, yaani kufikia mwaka 2025.

Mo, mbunge wa zamani wa Singida Mjini, pia alisema ataendelea kutoa misaada kwa jamii ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wake wa kurudisha faida kwa jamii.

Katika orodha hiyo ya mabilionea barani Afrika, Johann Rupert wa Afrika Kusini (70), amepanda kwa nafasi moja hadi ya nne, akifuatwa na Mike Adenuga wa Nigeria (70) ambaye mwaka jana alikuwa nafasi ya tatu.

Wengine wanaokamilisha orodha hiyo ya mabilionea 18 barani Afrika na nchi wanazotoka kwenye mabano ni: Abdulsamad Rabiu (Nigeria), Issad Rebrab (Algeria), Naguib Sawiris (Misri), Patrice Motsepe (Afrika Kusini), Koos Bekker (Afrika Kusini), Mohamed Mansour (Misri), Aziz Akhannouch (Morocco), Mo Dewji (Tanzania), Youssef Mansour (Misri), Othman Benjelloun (Morocco), Michiel Le Roux (Afrika Kusini), Strive Masiyiwa (Zimbabwe) na Yasseen Mansour (Misri).



MkuuwaJeshi la KujengaTaifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge (wa pili kushoto), akiwasaidia vijana wa jeshi hilo, kubeba kokoto kwa ajili ya kuchanganya zege, katika ujenzi unaoendelea wa skimu ya kilimo cha kimkakati cha umwagiliaj inayojengwa katika kikosi 837 Chita JKT, Ifakara, mkoani Morogoro juzi.**PICHA: RENATHA MSUNGU**.

# Magari ya serikali kutumia gesi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameagiza magari ya serikali, taasisi za umma, sekta binafsi na wananchi kujiandaa kutumia gesi asilia katika magari yao kwa kuanza kubadili mfumo wa magari yao kutoka matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli kuingia katika matumizi ya gesi.

Dk. Kalemani aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea kituo cha kusambaza gesi asilia kwenye magari kilichoko Ubungo na kubainisha kuwa gesi imeshaanza kutumika kwenye magari nchini na mfumo huo utaenezwa kwa kasi zaidi muda siyo mrefu.

Waziri huyo pia alikwenda Mtaa wa Nzasa, Sinza Wilaya ya Kinondoni kuzindua moja kati ya laini nne zitakazotumika kusambaza gesi asilia majumbani mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na wananchi wa mtaa huo kuhusu gesi asilia kutumika kwenye magari, Dk. Kalemani alisema tayari ameshatoa maelekezo kuwa itakapoanza, isiwekwe kwenye mabasi ya mwendokasi na magari ya serikali pekee, bali pia yale ya sekta binafsi na ya wananchi nayo yanufaike na nishati hiyo.

"Wenye magari pelekeni magari yenu maeneo ya kubadili mfumo wa petroli na dizeli na watu wa bodaboda na pikipiki nanyi mjiandae kutumia gesi asilia, itawasaidia kupunguza gharama za uendeshaji," alisema.

Pia, aliwataka wanaoagiza magari nje ya nchi, waagize yale ambayo tayari yapo kwenye mfumo wa gesi ili kuepuka gharama za kuyabadilisha ambapo hugharimu kati ya Sh. 800,000 hadi Sh. milioni moja kwa kila gari.

Kuhusu gesi asilia ya majumbani, Dk. Kalemani aliwatoa wasiwasi wananchi kuwa ni salama, haina madhara yoyote, hivyo itakapoanza, waitumie kwa sababu itawapunguzia gharama za matumizi, akibainisha kuwa uniti moja ni Sh. 1,000 na itanunuliwa kama luku.

Alisema ipo mifumo minne eneo la Ubungo Maziwa ya kusambaza gesi hiyo majumbani ambapo laini ya kwanza inaanzia Ubungo kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Makongo hadi Bagamoyo.

Alisema laini ya pili ambayo aliizindua jana, inatoka Ubungo Maziwa na kupita Mtaa wa Nzasa, Kijitonyama na kuelekea Mikocheni na ya tatu inatoka Ubungo kuelekea Tabata, Pugu na baadaye itafika Morogoro.

Alisema laini ya nne inaanzia Ubungo Maziwa na inakwenda Temeke, Chang'ombe, Kurasini hadi Mbagala.

Waziri huyo aliliagiza Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC), kuhakikisha laini zote nne za kusambaza gesi zinatumika.

"Mkandarasi (Kampuni ya wazawa BQ) vifaa vitakavyohusika kutandaza gesi hii kutoka hapa Nzasa vitoke Tanzania na ni marufuku kununua luku ya gesi, mabomba kutoka nje ya nchi, nikija Juni 23 mwaka huu, nisiambiwe mabomba hayajaja au luku haijaja, ninawapa miezi sita mkamilishe hii kazi na siyo miezi 12 iliyosemwa hapa," aliagiza.

Alisema Tanzania ina futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia na kwamba mpaka sasa matumizi ni trilioni 0.57 ambapo bado hawajafikia hata trilioni moja.

Alisema katika gesi hiyo, kiwango kilichotengwa kwa ajili ya nyumbani ni trilioni 1.17.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, shirika limetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuunganisha wateja wa majumbani wapatao 1,000 mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

## JKT kulima mpunga mara 2 kwa mwaka

**Na Renatha Msungu, MOROGORO**

KUTOKANA na mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji unaoendelea katika eneo la JKT Chita mkoani Morogoro, jeshi hilo limepanga kuendesha kilimo cha mpunga mara mbili kwa mwaka, ili kujitosheleza chakula katika kambi zake.

Mbali na hilo, jeshi hilo limesema ziada ya mazao itaingizwa katika ghala ya taifa.

Akizungumza jana wakati akitembelea mradi wa skimu ya umwagiliaji katika Kikosi cha 837 KJ Chita, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema ujenzi wa skimu hiyo hadi sasa umefikia asilimia 45, hatua ambayo ni nzuri kulingana na muda walioanza ujenzi huo.

"Nilivyokuja kutembelea Desemba mwaka jana, ujenzi ulikuwa asilimia 40, leo (jana) nimekuja imefika asilimia 45, hayo ni matokeo mazuri na tutafikia malengo tuliojiwekea kukamilisha skimu hii," alisema Meja Jenerali Mbuge.

Alisema kwa msimu huu, wameanza kwa kulima shamba la ekari 2,500 na mkakati wa JKT ni kupanua miundombinu hiyo ili kufikisha ekari 12,500 ifikapo mwaka 2025.

Alisema baada ya kukamilika kwa skimu, watakuwa na uwezo wa kulima mara mbili kwa mwaka, kwa sababu maji ya mito ambayo miundombinu imejengwa, hayakauki iwe kiangazi au msimu wa mvua.

Alisema kupitia mradi, JKT imetoa fursa ya kushirikisha jamii inayozunguka kambi hiyo kwa kuwapa ujuzi wa kitaalamu ambao unatumiwa na jeshi hilo kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika utaratibu mzima wa upandaji wa zao la mpunga.

"Tumeamua kuwashirikisha wanakijiji kwa sababu tunahitaji wajue ili nao wakaitumie teknolojia ya kilimo hicho uraiani, ili kuepuka kupoteza mbegu nyingi wakati wa kupanda," alisema Meja Jenerali Mbuge.

Alisema utekelezaji wa mradi umesaidia kwa kiasi kikubwa jamii inayozunguka kambi hiyo kupunguza adha ya mafuriko katika mashamba yao na badala yake sasa mfumo wa umwagiliaji kuelekeza maji sehemu moja.

Mbali na hayo, alisema baada ya mradi huo kukamilika, utatumiwa na baadhi ya wanafunzi wa vyuo watakaotumia skimu hiyo kwa mafunzo kwa vitendo.

Alisema wageni pia watakwenda kutembelea sehemu hiyo kama kivutio kutokana na mitaro mingine kupita chini ya reli.

Alisema wito wao kwa serikali ni kuwasaidia fedha ili wapanue miundombinu zaidi, ili kulima ekari 12,500, akibainisha kuwa serikali ni sikivu na wanaamini hilo litafanikiwa.

Mkulima Hamisi Kayoga alisema raia wamenufaika na kilimo hicho cha mkakati kinachoendeshwa na jeshi hilo.

Alisema kilimo hicho kimewapa manufaa makubwa kwa sababu teknolojia ya upandaji wanayoitumia atakwenda kuitumia uraiani.

Kayoga alisema wanaishukuru JKT kuamua kushirikiana nao katika kilimo hicho cha mpunga na wamepata fursa ya kujua kupanda kitaalamu zao hilo la biashara.

HABARI KITAIFA

# Tril. 18/- zapita miamala ya mtandaoni kila mwezi

**Na Prisca Ulomi, DODOMA**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameiarifu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuwa kiasi cha Sh. trilioni 18 kinapita kwenye mitandao kwa mwezi.

Alitoa taarifa hiyo juzi wakati wa kikao chake na kamati hiyo kilichohudhuriwa na wajumbe wa menejimenti ya wizara hiyo na wakuu wa taasisi zake ikiwamo Shirika la Posta (TPC), Shirika la Mawasiliano (TTCL), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA -CCC) na Tume ya TEHAMA (ICTC) kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Bunge jijini Dodoma.

Dk. Ndugulile aliwaambia wajumbe wa kamati hiyo kuwa takriban miamala milioni 300 inafanyika kwa mwezi mtandaoni na serikali inapata Sh. bilioni 80 kwa mwezi za tozo kutokana na fedha zinazopita mtandaoni na mzunguko huo wa fedha mtandaoni kwa mwezi.

Alisema miamala inayofanyika na tozo ambazo serikali inapata ni kutokana na kuwapo kwa matumizi ya TEHAMA.

Alifafanua kuwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni njia kuu ya uchumi na inawezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano yenye kasi, kufanikisha utendaji kazi wa mifumo ya TEHAMA na huduma za fedha mtandaoni na wizara imejipanga kuandaa ramani ya njia ya miundombinu ili kufanikisha mwingiliano wa ujenzi na upanuzi wake pale inapokutana na njia za miundombinu mingine kama vile ya barabara, maji, umeme na reli.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Moshi Kakoso, aliitaka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuongeza udhibiti na usimamizi wa huduma za mawasiliano kwenye suala la fedha mtandao, ili kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha na kuongeza mchango wa tozo serikalini zaidi ya Sh. bilioni 80 kwa mwezi kwa kuwa miamala mingi ya fedha inafanyika na fedha nyingi zinapita kwenye mtandao, ili TEHAMA iongeze mchango wake kwenye ukuaji wa uchumi na kuchangia zaidi pato la taifa.

Naibu Waziri, Kundo Mathew, alisema wizara itaipa ushirikiano wa kutosha kamati hiyo, ili kwa pamoja serikali kupitia wizara na Bunge, watekeleze majukumu yao kwa kuwa wote kwa pamoja wanamhudumia mwananchi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, aliwaeleza wajumbe wa kamati hiyo kuwa wizara itaendelea kusimamia na kuendesha vyema Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kunufaika na huduma za mawasiliano na TEHAMA inatumika kurahisisha maisha yao ya kila siku katika nyanja ya kiuchumi na kijamii.

## Ekari 150 kupandwa mbegu za mpunga

**Na Renatha Msungu, MLIMBA**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetenga ekari 150 za mashamba kwa ajili ya kuandaa mbegu za mpunga, ili misimu ijayo waanze kutumia mbegu kutoka ndani ya jeshi hilo na kuihudumia jamii inayowazunguka.

Akizungumza katika ziara yake katika mradi wa skimu ya umwagiliaji iliyoko Chita JKT, Kaimu Mkuu wa Utawala wa JKT ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mkakati, Mifugo na Uvuvi, Kanali Hassan Mabena, alisema katika msimu inayofuata, wamepanga kutumia mbegu zinazotoka ndani ya jeshi hilo.

Alisema mbegu hizo siyo tu zitatumika katika mashaba ya JKT, bali zitatumika kuhudumia pia mashamba ya jamii inayowazunguka kwa sababu zitakuwa na ubora kutokana na jinsi ambavyo zinatunzwa na wataalamu kutoka jeshi hilo wakishirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

"Tumejipanga misimu ijayo kuanza kutumia mbegu kutoka ndani ya jeshi, lengo ni kuzidi kupanua wigo wa kilimo mkakati tunachofanya," alisema Kanali Mabena.

Akizungumzia ujenzi wa skimu inayoendelea, Kanali Mabena alisema mpaka sasa tayari mabanio yote yameshakamilika, hivyo mradi huo unatarajia kukamilika Mei mwaka huu.

Alisema kazi ambayo imefanyika inalenga kuhakikisha maji yanayotoka kupitia mito, yatapita katika mifumo hiyo ambayo imejengwa katika mitaro mama na baadaye yatakwenda kufika katika sehemu ambazo wenyewe wanaita vigawa maji na kuelekezwa katika mashamba husika.

Alifafanua zaidi kuwa awamu ya pili ya mradi huo itakuwa ni kutengeneza mitaro ambayo itakuwa inaingiza maji shambani, mitaro mikubwa na midogo ambayo itakuwa inatoa maji yasiyohitajika.

ONESHA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akifurahia jambo na Kamishina Jenerali wa Uhamiaji, Anna Makakala (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela (wa tatu kulia) na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Khamis (wa tatu kushoto), baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji cha Boma Kichakamiba, wilayani Mkinga, juzi. **PICHA: OWM**.

# Waziri Mkuu aridhishwa na ujenzi Chuo cha Uhamiaji

**Na Mwandishi Wetu, MKINGA**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji cha Boma Kichakamiba kilichoko wilayani Mkinga mkoani Tanga.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na makamanda na wadau mbalimbali mara baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho katika ziara yake ya kikazi mkoani Tanga.

Ujenzi wa chuo hicho ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Oktoba mwaka jana wilayani humo wakati akimnadi aliyekuwa mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli.

Waziri Mkuu alisema ujenzi wa chuo hicho ni jambo jema katika Idara ya Uhamiaji na lina manufaa makubwa nchini.

Alisema ujenzi wa majengo hayo ni mwendelezo wa jitihada za serikali za kuhakikisha idara hiyo inafanya kazi kwa ufanisi.

"Katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano, zipo jitihada kubwa zimefanywa za kuimarisha miundombinu kwenye majeshi yetu.

"Kwenye Idara ya Uhamiaji, tumewezesha upatikanaji wa nyumba 103 za makazi pamoja na ujenzi wa jengo la makao makuu mkoani Dodoma," alisifu.

Waziri Mkuu aliagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ihakikishe inatenga mapema bajeti kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji, ili wakamilishe miundombinu ya chuo hicho.

Waziri Mkuu pia alipongeza Idara ya Uhamiaji kwa namna wanavyofanya kazi kwa weledi na kuibua mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wahamiaji haramu wanaoingia nchini bila kufuata utaratibu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Chilo, alisema kambi hiyo ya mafunzo ya maofisa na askari wa Idara ya Uhamiaji, ni matunda ya serikali kuboresha Idara ya Uhamiaji.

Naibu Waziri Chilo alisema ujenzi wa kambi hiyo yenye ukubwa wa ekari 395, utasaidia wananchi wa maeneo ya jirani kupata huduma muhimu za kijamii ikiwamo maji na umeme.

Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema lengo kuu la kuanzisha kambi hiyo ya kijeshi ni kutoa mafunzo ya utayari kwa wakati na gharama nafuu, kupata askari wenye ukakamavu, nidhamu, weledi na maadili ya kikazi ya kiuhamiaji.

Dk. Makakala alisema mpaka sasa wameshatumia Sh. milioni 140 katika ujenzi zilizotokana na michango ya hiari ya maofisa na askari wa uhamiaji waliochangia Sh. milioni 81 huku wadau mbalimbali wakichangia Sh. milioni 59. Alisema kambi hiyo kwa sasa ina uwezo wa kuchukua askari 300 kwa wakati mmoja na endapo watapata fedha, wanatarajia kuongeza uwezo wa chuo hadi kufikia askari wanafunzi 1,000.

Aliongeza kuwa idara hiyo inao mpango wa kuongeza majengo ya kudumu na kuwa na huduma muhimu za mabweni, zahanati, madarasa, nyumba za ibada na maktaba, ili kukifanya chuo hicho kuwa na hadhi ya kitaifa na kimataifa.

Alisema wanahitaji Sh. bilioni tatu ili kutekeleza mpango huo.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme (TANESCO) Mkoa wa Tanga, Juma Nkija, alipoitwa kueleza mpango wa kupeleka umeme chuoni hapo, alisema ndani ya siku tatu kuanzia jana, watawasha umeme katika eneo hilo.

Kuhusu suala la maji, Waziri Mkuu alimwita wa Mkurugenzi wa Ufundi wa RUWASA, Deusdedit Magoma, aeleze ni lini yatapatikana na akajibiwa kuwa wamepokea Sh. milioni 150 na ndani ya mwezi mmoja, maji yatakuwa yanapatikana chuoni hapo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaohujumu miradi ya maendeleo wasionewe haya

SERIKALI imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, nishati, miundombinu ya barabara na maji. Lengo la kutekeleza miradi hiyo ni kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Watanzania ili kuondokana na lindi la umaskini.

Katika sekta ya elimu, kwa mfano, serikali kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikijenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu na ununuzi wa madawati ili wanafunzi wasome kwa amani.

Sambamba na hilo, ujenzi wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali umepamba moto huku waziri na naibu wake, wakizunguzunguka nchi nzima kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati na wananchi wanapata huduma hiyo bila vikwavyo vyovyote.

Pamoja na miradi hiyo, kumekuwa pia na utekelezaji wa miundombinu ya usafirishaji kama vile barabara na reli ya kisasa. Barabara nyingi zimekuwa zikijengwa maeneo ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kusafiri kwa uhakika pamoja na kusafirisha mazao kutoka shambani hadi sokoni.

Katika jiji la Dar es Salaam, kwa mfano, kuna ujenzi wa barabara za mitaani na zile kuu ambazo zinajengwa kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari ambao kwa muda mrefu umeathiri shughuli za kila siku. Badala ya watu kuwaza kufanya kazi ili kujiletea maendeleo, walikuwa wakiwaza namna watakavyopambana na foleni, hivyo kujikuta muda mwingi wanatumia barabarani.

Hatua hiyo iliifanya serikali kutafuta namna ya kupunguza tatizo hilo. Miongoni mwa mbinu zilizotumika ni kuanzisha usafiri wa mwendokasi pamoja na kujenga madaraja ya juu TAZARA na Ubungo pamoja na kupanua barabara ya Ali Hassan Mwinyi kutoka Morocco hadi Mwenge na baadaye Mwenge hadi Tegeta. Hiyo ni mifano tu namna serikali ilivyojipanga kutatua tatizo hilo ndani ya jiji la Dar es Salaam.

Pamoja na jitihada hizo za serikali, kumekuwa na watu wasioitakia mema nchi ambao wamekuwa wakihujumu miundombinu hiyo ama kwa kung'oa mabomba, vyuma na kuiba vifaa vinavyotumika kwa ujenzi. Hatua hiyo imezorotesha kwa kiasi kikubwa juhudi za serikali katika kuwakomboa wananchi dhidi ya ukosefu wa huduma mbalimbali.

Hivi karibuni, kwa mfano, kumekuwapo na taarifa za watu kuhujumu mradi wa ujenzi wa barabara ya Morocco hadi Mwenge kwa kuiba reki zinazotumika kusambazia lami pamoja na malori mawili ya lami, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 80. Kadhalika kulipatikana habari za watu kukutwa na mataruma ya reli katika mradi wa reli ya kisasa (SGR), hatua ambayo ni uhujumu wa mradi huo.

Vitendo hivyo havipaswi kufumbiwa macho kwa sababu athari zake ni mbaya katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wahusika wa vitendo hivyo, wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria bila kuwaonea haya.

Kama wahenga wasemavyo, ukicheka na nyani utavuna mabua, ndivyo itakavyokuwa kwa watu wanaohujumu miundombinu ya miradi ya maendeleo ikiwamo kuiba vifaa. Watu hawa wakifumbiwa macho watasababisha madhara makubwa kwa jamii kwani wananchi watakosa huduma muhimu.

Ni vyema hatua kali zikachukuliwa dhidi ya watu wa aina hiyo ikiwamo kuchapwa viboko na kulipa fedha kwa uharibifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii iweke mipaka kati ya nadharia ya imani na afya

Na Sabato Kasika

KATIKA kuhakikisha huduma za afya zinaimarishwa, serikali imekuwa ikijitahidi kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali ili zitoe huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Jukumu hilo si la serikali tu, bali hata taasisi za kidini nazo kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya, zina hospitali zake, kwa lengo la kusaidiana na serikali kuboresha afya kwa waumini wake na Watanzania kwa ujumla..

Hiyo inaonyeha kwamba pamoja na kuwapo kwa huduma za kiroho, bado waumini wanahitaji kupata huduma za afya pale wanapougua, hivyo suala la kuwapo kwa mipaka kati ya nadharia ya imani na huduma ya afya ni muhimu.

Hapa maana yake ni kwamba, muumini anapougua anatakiwa kwenda hospitalini kupata vipimo na kisha matibabu, badala ya kwenda katika nyumba zsa ibada akiamini kwamba Mungu atamuwezesha kupona.

Kama ingekuwa hivyo, kusingekuwa na haja kwa taasisi za dini kujenga zihanati, vituo vya afya au hospitali. Lakini kwa kuwa kuna mipaka kati ya nadharia ya imani na afya, taasisi hizo nazo zinatoa huduma za afya.

Pamoja na hilo, kumekuwapo na dhana iliojengeka miongoni mwa waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini ambao wamefikia hatua ya kutokwenda hospitalini pale wanapougua, wakiamini kwamba wamekokoa, hivyo inatosha.

Kwa dhana hiyo, wanaweza kujikuta wameumia, hivyo ipo haja watafakari kwa kina na kuchukua hatua sahihi, wakitambua kuwa ni muhimu kuwa na mipaka kati ya nadharia ya imani na dini na suala zima la afya.

Dhana hiyo ndiyo inayomwibua ni Mchungaji na Nabii Dk. Enock Mwasambogo na kuitolea ufafanuzi kwa waumini wake kwamba, hamuungi mkono mgonjwa anayeacha kutumia dawa kwa madai ya kuokoka.

Hivi karibuni akihubiri kwenye ibada, Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, alisema katika maandiko, hakuna mahali ambapo Mungu anataka watu waliookoka wasiende hospitalini au wasitibiwe.

Alisema walioambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU0 na walioanzishiwa dawa za kufubaza virusi hivyo, baadaye wakaamua kuokoka, waendelee kutumia kama kawaida, wasidhani kwamba kuokoka ni tiba tosha.

Hoja ya mchungaji huyo ni ya msingi kwa kuwa anasema wagonjwa wanaokwenda kanisani hawatakiwi kupuuzia ushauri wa madaktari wakati uponyaji wa Mungu ukiendelea. Kimsingi inauma anaposema watu wengi wanakufa kwa imani ambazo hata Mungu mwenyewe haziungi mkono, na kwamba mtu akiwa na malaria, anapewa dawa kunywa umalize dozi, asitupe kwa kuwa umeokoka.

Mtumishi huyo wa Mungu anaamini kuwa muumini akicheza atakufa, na kutaka mambo ya rohoni yafanyiwe kazi kiroho na ya mwilini yafanyiwe kazi kwa njia bora za mwilini ili Mungu naye ayabariki. Kama wapo wale ambao wameambukizwa VVU na kuanza kutumia ARVs na kisha wakaacha, kwa sababu wameokoka, kuna haja ya kuwauliza. Je, kwa nini taasisi za dini zina zahanati, vituo vya afya na hospitali?

Ni vyema watu wenye mtindo huo wakiajua kuwa, taasisi hizo zinatoa huduma za afya, kwa vile zinatambua kwamba, mambo ya kiroho yanashughulikiwa kiroho, na mambo ya kimwili yanashughulikiwa kimwili.

Msingi mkubwa hapa ni kutambua mipaka kati na nadharia za imani na umuhimu kujitibia pale muumini anaugua ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza iwapo mgonjwa atazidiwa.

Ikumbukwe kuwa Tanzania ina Sheria ya UKIMWI iliyopitishwa na bunge mwaka 2008, ambayo inaelekeza mambo mbalimbali muhimu yanayohusu mtu aliyeambukizwa VVU na jinsi anavyotakiwa kufanya.

Sheria hiyo ni mahususi ili kuzuia maambukizo ya VVU, kuendeleza na kutunza afya ya jamii, na inatoa mwongozo wa huduma inayotakiwa kwa watu walioambukizwa au kwa wale walio katika hatari ya kupata maambukizo.

Inataja haki za anayeishi na VVU kuwa ni kupata huduma za afya ya mwili na akili kwa kadri ya ubora unaohitajika, matibabu sahihi ya magonjwa nyemelezi na kupata haki zote za binadamu mwingine yeyote ambaye hajaathirika.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Hii ndiyo dawa ya wenzetu wanaohujumu miundombinu

KITENDO cha baadhi ya wenzetu kuiba viti vya shule na kuviuza kama vyuma chakavu kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni kinatia kinyaa.

Pia kitendo cha wenzetu walioaminiwa ofisi za umma kuuibia umma ni mauaji, hujuma na unyama visivyo na kifani. Vinatia kinyaa. Rejea kufukuliwa kwa wizi wa madawa kwenye hospitali ya rufaa ya Muhimbili hivi karibuni.

Je, mchezo huu unafanyika Muhimbili tu au ni nchi nzima? Je umekuwa ukifanyika kwa muda gani na fedha kiasi gani tushapoteza kama taifa? Japo wote tungependa tutajirike, vitendo kama hivi, ni zaidi ya ujambazi.

Ni ujambazi, unyama na uuaji wa wazi. Ni vya kikatili; na vinapaswa kupigwa vita kwa ukali wote. Je, ni watu wangapi wasio na hatia wamepoteza maisha kutokana na ukatili huu utokanao na ubinafsi, ulafi, upofu na upogo wa kutisha? Je, kama taifa tunapaswa kufanya nini kupambana na ushetani huu ambao kama siyo kuigaiga na kuendekeza haki za binadamu zinazokinzana na za wengine wanaopatikana na hatia kama hizi ni wa kunyonga ili liwe mfano na somo kwa wengine wanaootea na kuurudufu kwa kutaka kutimiza tamaa zao za utajiri.

Ukiachia mbali jinai tajwa hapo juu kuwa unyama, ni uhujumu wa nchi na uchumi. Kutokana na hasira na machukizo jinai hizi zinasababisha, hata pale wahusika wanapokutwa na hatia, mojawapo ya adhabu iwe ni kuwachapa bakora za kutosha hadharani halafu mengine yafuatie. Kwanini taifa letu linaanza kugeuzwa la mahayawani wa kutisha hivi? Yaani pamoja na juhudi za Rais John Pombe Magufuli kuondoa nchi kwenye utegemezi na umaskini bado kuna viumbe wanaofanana na binadamu waliogoma kumuelewa! Inatisha na kusikitisha.

Ngoja tugusie jinai na kadhia ya uhujumu uchumi vitokanavyo ubinafsi na ulafi wa kutisha kwa ujumla. Tunapogundua jinai na kadhia kama hizi, tuangalie waliotenda ni nani na wamesukumwa na nini. Wapo wanaosukumwa na ujinga na umaskini vya kawaida. Mara nyingi, ujinga na umaskini vikichanganyika, vinazalisha viumbe wa ovyo hata kuliko mbwa. Maana, mbwa mwenye akili zake, hawezi kumuibia anayemfuga kwa vile anajua wajibu wake. Je, binadamu anayehujumu miundombinu na mali nyingine kama vile shule, mabomba ya maji, barabara, reli na mingi tena vyake, siyo wa ovyo kuliko mbwa asiyemwibia anayemfuga? Mbwa ni hayawani. Lakini hayawani anayejua umuhimu wa amfugaye anaweza kuwa mwema na wa maana kuliko binadamu asiyejua umuhimu wa huduma apewazo na serikali yake tena kwa kodi kubwa za wengine.

Tunapopata maskini wa majinga kama hawa, kamata, charaza bakora na toza faini eneo zima linapotokea tukio ili kila mmoja aonje madhara ya kuendekeza ujinga, umaskini na njaa. Hivi kweli kuna haja ya kuiba vifaa vya umeme, mabomba ya maji, kutupa taka na kuziba mifereji na kuchafua mito yetu, kuhujumu reli au barabara na mengine kama haya wakati serikali inaingia gharama kubwa kuviweka ili kuondoa kero kwa wale wale ambao miongoni mwao wanavihujumu? Kwa mfano, kama bomba la maji la kijiji limehujumiwa, wanakijiji wapewe fursa kwanza, kuwasaka au kuwataja wahusika. Wasipowapata, wote wawajibishwe kwa kuchangishwa fedha za kurejesha bomba au kitu husika.

Adhabu pekee haitoshi kukomesha tatizo. Lazima serikali kwa makusudi mazima itoe elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa miundombinu kwa maisha na ustawi wao, gharama za kupatikana miundombinu na madhara kwa watu binafsi, jamii na taifa. Sambamba na umuhimu, elimu husika ieleze bayana madhara yatokanayo na hujuma hizi kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Katika kutekeleza hili, lazima kuwapo na usimamizi na ulinzi shirikishi ambapo kila mdau ana wajibu wa kulinda mali za umma akiwa ni sehemu ya umma. Lazima wananchi waambiwe kuwa wao ndiyo serikali na serikali siyo kiumbe cha ajabu tofauti na wao.

Lazima wananchi wafundishwe kuwa wao ni walinzi na wanufaikaji wa mali wanazohujumu kwa maslahi binafsi. Wananchi wakitishwa jukumu la kulinda miundombinu na mali za umma, watavidumisha.

Kwani, wanajuana kwa majina na sura ukiachia mbali shughuli wazifanyazo mbali na tabia za wenzao. Mjenga na mbomoa nchi ni mwananchi na mnufaikaji kadhalika. Hili lazima walijue na kulikubali.

Tumalizie kuwa wenzetu wa nchi za Magharibi hawakufikia hali ambayo hutufanya kuwahusudu kimiujiza bali ni kwa kubanana hadi wakazoea baada ya kuona manufaa ya kuwa na miundombinu endelevu na ya kudumu kutokana na kuilinda vilivyo na kuitumia vizuri. Mwisho, piga marufuku biashara zinazopokea vitu kama vyuma chakavu na mengineyo.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Soma ujiajiri inapasua kichwa!

HAKUNA kitu kinachosumbua vichwa vya watu kama mtihani. Mtihani wa kitu chochote ambacho mwishowe ni matokeo ya jinsi mtahini walivyofanya.

Wasiwasi huwajaa sana watahiniwa wanapokaribia siku za mitihani, si shuleni wala vyuoni, si sehemu za kazi. Mtihani ni pamoja na usaili wowote uwe wa ajira au wa polisi.

Lakini matokeo mazuri ya mitihani, huzalisha furaha isiyo na kifani kwa mhusika. Ndiyo sababu hata zawadi hutolewa kwa aliyefanya vizuri kwenye mtihani wowote, na mfaulu hujisikia vema sana.

Hakuna mzazi anayesikitika anapoambiwa mwanao kafaulu mtihani hata uwe wa darasa la saba. Mzazi hufunguka na hata kama hana kitu, hujikamua ili kuonyesha furaha yake na kumzawadia mtoto.

Furaha haishii ngazi ya familia, bali hufika hata ngazi ya kitaifa, ambapo wahusika wanaosimamia elimu hujisikia faraja zaidi wanapoona wanafunzi wamefaulu mitihani yao, na ndiyo sababu kila mwaka watatoa alama za ufaulu kwa asilimia.

Hujisikia vema sana waonapo ufaulu wa mwaka huu umepita wa mwaka uliotangulia, na kujipa matumaini kwamba kiwango cha elimu kimepanda ama kutokana na walimu kufundisha vizuri au wanafunzi kujibidiisha, au yote.

Zamani mtoto alipofaulu, mzazi alijipa matumaini ya ukombozi kwamba tayari anaandaa mtu ambaye atamaliza masomo yake na hatimaye apate ajira, amsaidie pamoja na familia nzima.

Enzi hizo hata aliyemaliza darasa la saba alipata ajira, kama si ualimu hata kazi ya jeshi ilimhusu. Hivyo ilikuwa faraja sana kuona mtoto akimaliza shule na kupata ajira na kujitegemea.

Vivyo hivyo kwa aliyemaliza darasa la 12 na aliyehitimu la 14; leo utasikia fomfoo au fomsiksi. Ilikuwa neema sana kwa mtoto kuvuka kote huko na kufikia chuo cha kati au kikuu, kwani uhakika wa kazi yenye maslahi makubwa ilikuwa dhahiri.

Ni wakati huo ambapo wahitimu wa darasa la saba mpaka vyuo vikuu, hawakuwa wakionekana mitaani wakisaka ajira! Haikuwa hivyo, kwani aliyemaliza darasa la 12 alitakiwa kujaza fomu maalumu za ajira, kwa kuwa ilikuwa lazima aajiriwe. Vivyo hivyo kwa darasa la 14.

Enzi hizo wahitimu hao walikuwa wachache, kwa kuwa shule zenyewe hususan za sekondari nazo zilikuwa chache. Kwa hiyo waajiriwa walikuwa wachache huku nafasi zikiwa nyingi, hususan serikalini.

Ndio wakati ambao serikali ilikuwa ina kila kitu, kuanzia shule, vyuo, ofisi za kiutawala, viwanda na mashirika. Hivyo wahitimu wote walimezwa humo. Kwa kifupi ajira zilikuwa za uhakika, ili mradi umalize shule au chuo kwa ufaulu uliotakiwa.

Polepole mambo yalianza kubadilika. Wanafunzi wakawa wengi katika shule za msingi, wahitimu wa darasa la saba wakaongezeka, wakati ambao ajira zikawa zinawatazama wa sekondari zaidi na vyuo.

Kana kwamba haitoshi, polepole hivyo hivyo, wahitimu wa sekondari nao wakaongezeka. wale wa fom foo nao wakajaa mitaani, ajira zikaenda kwa fom siksi. Kidogo kidogo wa fom siksi nao wakatupwa na wakati, ukimaliza hakuna kujaza fomu za ajira (Sel Forms), ajira zikawa za vyuo vya kati na kasha vyuo vikuu.

Hivi sasa inaonekana dhahiri wa vyuo nao wametupwa na wakati. Hivi sasa maliza rudikwa baba na mama yako, hangaika mwenyewe. Huku ukisikilizia mirindimo ya nyimbo za “jiajirini...msisome mkitarajia kuajiriwa na serikali...kuweni wajasiriamali...”

Nyimbo hizo hivi sasa zimezoeleka, huku mafunzo yatolewayo vyuoni hayawaandai wengi kujiajiri, kwa sababu mfumo wao bado ni wa kuajiriwa serikalini. Walimu, madaktari, wahandisi, watawala, na kadhalika. Ndiyo bado wanafundishwa vyuoni na kutakiwa kurudi nyumbani kujiajiri!

Itafika wazazi wataanza kuona elimu ni kupoteza muda na fedha, bora mabinti waolewe kama ilivyokuwa zamani au mabinti wabaki nyumbani kuchunga mifugo, kwa kuwa hata wakienda huko kunakoitwa vyuo, hatimaye watarudi nyumbani kutafuta cha kufanya.

Wenye dhamana waangalieni nini cha kufanya kuhusu elimu yetu, ili iwaandae watoto kuwa na cha kufanya kinachoendana na miaka wanayotumia wakiwa vyuoni. Tunashindwa nini wakati tuko katika uchumi wa kati bhana? Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# TARURA Mbulu mmelala usingizi wa pono



Na Thobias Mwanakatwe

NI Januari 17, 2021 naanza safari yangu kutoka Karatu Mjini kwenda Wilaya ya Mbulu mkoa wa Manyara.

Inanichukua takribani saa mbili kutoka Karatu hadi kufika Mbulu mjini ambako usafiri unaotumika huku ni magari aina ya Toyota Land Cruiser.

Nawauliza wenyeji wa wilaya hizi za Mbulu na Karatu ni kwa nini usafiri unaotumika huku ni Toyota Land Cruiser, wananiambia hii ni kutokana na hali ya barabara katika wilaya hizo kwa kuwa magari mengi yanapata shida sana.

Baada ya kufika Mbulu saa 11:00 jioni, nikaanza safari yangu kwenda kijiji cha Tsaayo kilichoko kata ya Kainam ambako inanichukua takribani dakika 40 kufika katika kijiji hicho kwa kutumia usafiri wa pikipiki ambao ndio pekee unaotumika.

Japo kutoka Mbulu mjini hadi Tsaayo hakuna umbali mrefu, nauli ya pikipiki ni kubwa mno ambayo ni Sh. 8,000 hali inayosababisha baadhi ya wananchi kushindwa kufika Mbulu mjini kutafuta mahitaji muhimu.

Kabla ya kufika Tsaayo unapitia kitongoji cha Tlawi, kitongoji cha Giroay ambako wakazi wa maeneo ni wakulima wa maharage ambalo ndilo zao kuu la biashara wanalolitegemea.

Mazao mengine wanayolima ni mahindi, alizeti na mbaazi na pia wanajishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na wa kienyeji.

Nikaanza kumdodosa dereva wa pikipiki aliyenichukua, mbona barabara hii ya kutoka Mbulu mjini hadi Tsaayo ni mbovu sana, akafunguka kuwa haijatengenezwa kwa zaidi ya miaka mitatu ndiyo maana imeharibika hivyo.

Kiukweli, barabara hiyo ni mbovu sana kiasi kwamba ukiwa umepanda pikipiki unahitaji kumshikilia sana dereva kiunoni ili kupata 'balance', vinginevyo unaweza kujikuta unadondoka.

Baada ya kufika tu Tsaayo, wenyeji wangu wananipokea na kitu cha kwanza wananipa pole kutokana changamoto ya barabara. Wakasema barabara yao hiyo ambayo ipo katika jimbo la Mbulu haijatengenezwa kwa muda mrefu na kero hiyo wanaijua viongozi akiwamo mbunge wao.

Kutokana na kero hiyo, ndipo nikakumbuka hivi ni nani mwenye mamlaka ya kutengeneza barabara za vijijini, kumbukumbu zikanijia kuwa ni Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini ( TARURA) ambayo iko kila wilaya.

TARURA ulifunguliwa rasmi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Kassim Julai 2, 2017. Uzinduzi wa TARURA ulifuatiwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.GN 211 ya 12 Mei 2017.

Lengo la kuanzishwa kwa TARURA ni kutoa matengenezo endelevu na gharama nafuu na maendeleo ya mtandao wa barabara vijijini na mijini ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii nchini Tanzania.

Pamoja na malengo hayo, TARURA Wilaya ya Mbulu bila kumung'unya maneno naweza kusema kazi imewashinda barabara nyingi za vijiji ni mbovu sana yaani kwa tafsiri nyingine ni kama wamelala usingizi wa pono.

Tatizo la watendaji kushindwa kuwajibika katika majukumu yao linaweza lisiwe ni kwa wilaya ya Mbulu tu bali linaonekana kuwa kama ugonjwa hususani kwa watumishi wengi waliopo wilayani ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea.

Kutokana na tabia hizo ambazo kimsingi haziwafurahishi viongozi wa juu wa serikali, ndiyo maana mara nyingi Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri wanapofanya ziara mikoani na wilayani, utasikia watendaji fulani wametumbuliwa ni kwasababu wanashindwa kuwajibika vyema katika kazi zao.

Japo sifahamu bajeti ya TARURA Mbulu katika matengenezo ya barabara, lakini nachokisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, imekuwa ikijitadi kutoka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya barabara.

Kwa msingi huo, watumishi wa TARURA Mbulu msipende kukaa ofisini mkinywa chai na vitafunwa, mkajisahau kwamba mna wajibu wa kutengeneza barabara za vijijini ili kuinua uchumi wa wananchi wa maeneo hayo.

Watumishi wa TARURA Mbulu kama kazi imewashinda, ingekuwa busara kama mtachukua uamuzi wa kujitumbua badala kusubiri kutumbuliwa kwa aibu kwa kushindwa kuwajibika vyema katika majukumu yenu.

Waziri Mkuu wakati anazindua aliagiza TARURA kushughulikia usimamizi mbovu wa mikataba ya ujenzi kati ya makandarasi na mamlaka katika miradi ya barabara, kusisitiza juu ya uwazi katika mikataba yote ya kazi za umma.

Aliwaonya baadhi ya viongozi wa halmashauri za wilaya ambao walishutuhumiwa kwa kubadilisha matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya barabara kwenye miradi mingine, alisema fedha zinapaswa zitumiwe kwenye miradi iliyopangwa.

Pia alisema TARURA itawezesha maboresho kwenye mtandao wa barabara za vijijini na mijini, na kuwezesha watu kusafirisha mazao na vitu vingine kutoka vijiji hadi maeneo ya mijini.

TARURA Mbulu tambueni kuwa wananchi wa vijijini, kikiwamo cha Tsaayo, wanayo haki ya kupata barabara nzuri ili kusafirisha mazao yao kupeleka katika soko kuu la Mbulu mjini.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU KIBARIKI KIJIJI CHA TSAAYO.**

***Kwa maoni na ushauri tuwasiliane katika baraua pepe mwanakatwe2015@gmail.com barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA

# Fahamu nafasi, wajibu wa mke katika ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

MPANGO wa asili wa Mungu kuhusu ndoa ni mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu. Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane kwani kila mmoja anacho cha kuchangia katika uhusiano na maisha yao. Mwanamume na mwanamke wanategemeana.

Pamoja kwamba wajibu na majukumu yao yanatofautiana, wote wako sawa kwa umuhimu. Wote ni watu muhimu katika kujenga familia na jamii iliyo bora.

Yafuatayo ni majukumu ya mwanamke katika ndoa:

**Kumsaidia mume**

Mke ni msaidizi wa mume wake katika maisha na majukumu yake, hivyo kumsaidia na kumtia moyo mume katika majukumu yake ya kutunza familia ni wajibu wa msingi wa mke. Wanawake wanao uwezo na nafasi kubwa ya kumfanya mume afanikiwe au asifanikiwe katika majukumu yake. Kwa hiyo, kufanikiwa au kushindwa kwa mume kunategemea aina ya mke aliye naye.

**Mlinzi na mtetezi wa mume**

Mke anao wajibu wa kutunza udhaifu wa mume wake, kulinda heshima yake na kuwa msemaji wake. Hii inatokana na ukweli kwamba wanawake wamepewa uwezo wa kuzungumza maneno mengi zaidi kuliko wanaume. Kinababa wakijua kuishi vyema na wake zao, watapata raha na kuongeza siku zao za kuishi duniani.

**Mlezi mkuu wa ndoa**

Mlezi mkuu wa ndoa ni mke. Hili ni jukumu kubwa la kijamii ambalo Mungu amempa mwanamke kwa sababu ya nguvu ya ndani ya kulea na kukuza; hamasa na ushawishi alivyonavyo mwanamke. Mwanamke anao uwezo na nguvu ya kubadili mambo au mtu. Ni muhimu wanawake watambue kile Mungu alichoweka ndani yao.

**Kutii na kumheshimu mume**

Hili ni hitaji muhimu la mwanamume.Wanaume wanapenda kuheshimiwa. Hawapendi kudharauliwa na wanamke wala kuwa na majibizano nao. Mke akimheshimu mume wake, kwa vyovyote, watoto nao watamheshimu baba yao kwani wanawake wanayo nguvu kubwa ya ushawishi kwa watoto.

Mwanamke mnyenyekevu na mwenye busara huwa hapendi kushindana na mume wake bali hutafuta njia bora ya kumaliza tofauti zao kwa amani. Kimsingi, hakuna mwanamume mkorofi mbele ya mwanamke mnyenyekevu.

**Kujali na kutunza nyumba**

Mke ajishughulishe na mambo ya nyumba yake kwani nyumba ni mwanamke. Yeye ndiye malkia wa nyumba yake. Mama akifurahi, nyumba nzima inafurahi. Akikasirika, nyumba inageuka kuwa jehanamu.

Mwanamke ndiye wa kuifanya nyumba iwe nyumbani, yaani mahali panapovutia kukaa. Pamoja na majukumu ya kikazi waliyonayo baadhi ya wanawake, majukumu hayo yasiondoe nafasi na wajibu wa kuwa mke.

**Kutunza usafi wa roho, nyumba na mwili.**

Mwanamke ni ua la nyumba. Mwanamke usafi. Baadhi ya wanawake wameolewa lakini hawajui kutunza ustawi wa nyumba zao. Hawajui kutunza waume zao; hawajui kupika; hawatunzi usafi wa nyumba zao, mazingira yake, na miili yao. Baadhi yao wana kauli mbaya kwa waume zao.

Hali hii imesababisha baadhi ya waume kuwaepuka wake zao. Kwa hiyo, ni muhimu mke ajiweke katika mazingira ya kuwa kivutio kwa mume wake kwa kauli, matendo na mwonekano. Hata pale mwanamume anapokuwa mchafu na hajui kupika, hupenda mwanamke msafi na mpishi mzuri.

Kimsingi, wanandoa wakitambua nafasi na wajibu wao, na kila mmoja akitimiza wajibu wake ipasavyo, hakika ndoa zitakuwa imara na zenye mvuto. Makazi ya wanandoa yatakuwa maskani ya Mungu na baraka.

Ili haya yote yawezekane, uhusiano wa wanandoa na Mungu na nia ya kupenda kujifunza ni muhimu sana. Mungu ndiye hutupa nguvu ya pekee ya kuweza kuzikabili changamoto na kuwa watu wema.

Anayependa kujifunza, anatamani mabadiliko ndani yake. Mungu akusadie!

***Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.***

MAISHA
JANUARI 24, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 10

**Mwisho wa urafiki na mwanao huanzia hapa...**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba



## KIPAIMARA

Ukurasa 12



UWEKAJI 'WEAVING'

# Urembo unaosumbua wengi

Ukurasa 14

# Mwisho wa urafiki na mwanao huanzia hapa...

Na Moses Ismail



ANAPOKUWA mchanga, baba huonyesha mapenzi makubwa kwake na anatenga hata muda wa kurudi nyumbani mapema ili kucheza naye. Haijalishi awe mtoto mwanamke au mwanamume.

Hili linaendelea hata anapotimiza miaka minne na pengine hata mitano, na wakati mwingi baba akiwa kwenye 'baraza' na marafiki zake, huwapa 'stori' za mtoto wake kuhusu mambo fulani ya kitoto anayofanya.

"Mwanangu bwana, jana kanifurahisha sana." Atapigastori na wenzake akiwaeleza kituko fulani alichofanya mtoto wake na wenzake nao watacheka.

Na baba huyu huyu anapokaa sebuleni, pengine kusoma gazeti au kaangalia TV, haoni kero kabisa pale mtoto huyu anapomdandia mapajani na kuanza kumuongelesha au kumuuliza maswali fulani ya kitoto, atamjibu kitoto pia.

Tatizo linaanza pale mtoto anapoongezeka umri, unapofikia miaka sita na kuendelea, ule urafiki baina ya mtoto na baba unaanza kupungua kabisa. Baba anapoteza kabisa ile hamu ya kukaa na mtoto wake.

Maswali na michezo au kitendo cha mtoto kukaa pembeni mwa 'ubavu' wa baba wakati baba akiwa sebuleni, inaanza kuwa kero kwa baba, atamwambia: "Hebu kaa pale, tunagusanagusana nini? Huwezi kukaa pake yako?"

Haiishi hapo, ile tabia ya kumwambia kwa upole; "angalia shati lako lilivyochafuka, haya nenda kavue," sasa inabadilika, baba anapoteza upole wake na kuanza kusema: "Uona unavyojichafua, hebu toka hapa."

Hili linaongezeka kwenye jambo moja, la pili na baadaye linakuwa la kawaida kwa kila jambo analokosea mtoto, hakanywi tena kwa upendo, anakuwa wa kufokewa na kwa sababu hiyo anaanza kujiweka mbali na baba.

Hapa ndipo unapoanza kushangaa na kujiuliza, hivi ulifia wapi ule upendo baina ya baba na mtoto ulioanza tangu siku ile mtoto alipozaliwa na ukaendelea kuwepo mpaka mtoto alipokuwa na miaka mtano au hadi sita? Nini kimemkumba baba huyu?

Kiasili wazazi wote, hasa baba, wanapenda kuona mtoto wao wanaoanza 'kujitegemea' kwa mambo madogo kama kuomba maji au kuvua nguo wakati wa kujisaidia, wanaamini watoto hao wanaakili za kufanya mambo mengine.

Wanapoona mtoto anafanya makosa, ya kitoto, akiwa na umri huo wa kujitegemea, wanahisi wanafanya mambo hayo kwa makusudi na hapo ndipo urafiki wa utotoni baina ya mtoto na baba, pengine hata mama, unapokufa."

Katika hali kama hiyo, inawezekana kweli mzazi akaendelea kupatana na mtoto wake na kumpenda tena kama alivyokuwa mtoto mchanga au alipokuwa chini ya miaka minne?

Inawezekana iwapo wazazi watafahamu kuwa mtoto anapokuwa katika umri wa miaka 0 hadi miaka 14, akili bado inakuwa haijakomaa vizuri kuweza kuzingatia mambo kama watu wazima, ni kipindi ambacho watoto hufanya makosa mengi na wanahitaji kuvumiliwa.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Jinsi ya kuelezea furaha ya kumjua mtu, baada ya kutambulishwa.**

#Je suis ravi(e) de faire ta (votre) connaissance – Nina furahi kukufahamu.
#Ravi(e) de faire ta (votre) connaissance – Ni furaha kukujua.
#Je suis heureux(se) de te connaitre – nina furaha kukujua.
#Heureux(se) de te connaitre – Furaha kukujua.
#Je suis enchante(e) de faire ta connaissance – Nina furahi kukufahamu.
#Enchante(e) – Nimefurahi.
Le gendre – jinsia: Katika lugha ya Kifaransa, nomino zote lazima ziwe ama za jinsia ya kike (feminine) au jinsia ya kiume (masculin).

**Jinsi ya kike hupatikana kwa kuongeza herufi e mwishoni mwa nomino ya jinsia ya kiume lakini sio maneno yote ya yenye herufi e mwishoni ni ya jinsia ya kike.**
Masculin
un ami
un marchand un ours
un musicien le lion
le paysan
un vendeur un instituteur un boulanger mon pere mon frère
un patissier
Feminin
une amie
une marchande une ourse
une musicienne la lionne
la paysanne une vendeuse une institutrice une boulangere ma mere ma soeur
une patissiere

**Umoja na wingi wa maneno yafuatayo.**
Singulier
une femme un homme un cahier un tuyau
un bateau un cheveu un caillou un bocal
un soupirail
Pluriel
des femmes des hommes des cahiers des tuyaux des bateaux
des cheveux des cailloux des bocaux des soupiraux


**Sentensi zifuatazo haziko kwenye mpangilio maalum, zipange katika mtiririko utakaozifanya ziwe na maana kamili.**
t'appelles comment tu?
Comment t'appelles – tu?
est quel le nom de copain votre?
Quel est le nom de votre copain?
s'appelle Britney elle Elle s'appelle Britney
ta enchantee suis connaissance faire de je. Je suis enchantee de faire ta connaissance.
Paris travaillons a nous. Nous travaillons a Paris.
Elle amies habite ses chez. Elle habite chez ses amies.
Nous Mascara de sommes. Nous sommes de Mascara.
souhaitons vous la bienvenue en nous Tanzanie. Nous vous souhaitons la bienvenue en Tanzanie.

**Jitambulishe kutokana na huo mfano hapo chini (badili taarifa zisizokuhusu na zingatia jinsia).**
Je m'appelle Makame, je suis ne le 11 juillet 1997 a Iringa. Je suis Tanzanien. J'habite a Mtwara. Je suis eleve en troisieme annee secondaire. Je veux devenir ecrivain.

**Kamilisha sentensi hizi kwa viwakilishi vinavyofaa**
Je suis russe
Elle est francaise
Nous sommes tanzaniennes Vous etes anglais
Il est canadien
Tue s belge
Elles sont bresiliennes
Ils sont parisiens

## WATOTO

## PAKA RANGI




CHEKA

Alichokifanya daktari

JAMAA mmoja alipeleka redio yake kwa fundi kwa ajili ya kutengeneza, ilipofunguliwa ili itengenezwe ghafla wakatoka mende wengi na kusababisha jamaa kushtuka na kisha akasema "Kamata hao watangazaji wanakimbia"

SWALI
Mto Rufiji unapita katika mikoa mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Umerudi likizo, unamkuta mwanamke mwingine katulia tuli nyumbani kwako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vyetu vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita tulimsikia jamaa akilalamika mkewe kumfanyia vituko vya kutosha. Simu anachat na wanaume zake ikiwa sandukuni, chakula anapikia watoto usiku kati ya saa sita na saba, akiulizwa kwanini anatimkia kwao.

Hakika kila familia ina jaribu lake. Usione watu wakiwa na muonekano wa furaha barabarani. Wengine wanajikaza tu kwani yanayowasibu huko majumbani mwao ni balaa tupu. Yaani wanajikaza kisabuni kama wasemavyo walimwengu.

Hebu sikia mapito ya familia hii nyingine ambayo ilikuwa na maisha mazuri lakini shetani akaingilia kati na kuisambaratisha. Hivi majuzi nilisikia ushuhuda wa mama mmoja aliyetelekezwa na mumewe huku akimwachia watoto wanne.

Ni mama aliyeishi na mumewe kwa uaminifu na upendo mkubwa tangu mwanzo wa ndoa yao. Walioana wakiwa na maisha duni sana, lakini kwa sababu ya upende waliweza kuvumiliana, huku wakifanya kazi kwa bidii usiku na mchana. Mungu aliwabariki wakawa na mali nyingi, mifugo na miradi mingine.

Baada ya kupata mali, mume aligeuka na kuwa kichomi kwa mkewe, akawa anampiga, kumtesa na kumletea wanawake wa kila aina kwenye nyumba yao.

Yule mama alijaribu kuvumilia hali ile kwa muda mrefu kutokana na ukweli kwamba mumewe hakuwa na tabia hizo mwanzoni. Aliamini mume angebadilika na kuwa kama alivyokuwa zamani.

Kumbe hakujua kuwa mumewe tayari amepagawa na roho ya ufuska. Siku moja huyo mume akamchukua mkewe na watoto na kuwapeleka nyumbani kwa mkewe, akidai kuwa walikuwa hawajaenda kusalimia wazazi wao kwa muda mrefu. Pasipo kujua mawazo ya mumewe, yule mama aliwakusanya watoto na kwenda kijijini.

Baada ya siku mbili za kukaa wote kijijini, mumewe aliaga na kuomba arudi mjini ili aendelee kusimamia majukumu ya kazi. Waliagana vizuri bila ya hali yoyote ya mashaka kuonekana. Baada ya wiki tatu kuisha, yule mama aliwaomba wazazi wake arudi mjini kwani likizo ilikuwa imeisha na watoto walipaswa kurudi shuleni.

Wakati huo akiwa kijijini, mama huyu alikuwa akiwasiliana na mumewe bila tatizo. Hakuweza kujua mipango ya siri ya mumewe dhidi yake. Ama kweli, Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mama aliporudi nyumbani kwake, hakuamini alichokikuta. Alipatwa na mshangao kuona mwanamke mwingine kaletwa kwenye nyumba yao kama mke. Huyo mwanamke akawazuia wasiingie ndani.

Alipojaribu kumpigia simu mumewe, ilikuwa haipatikani. Mama alihisi kuchanganyikiwa kwani hakuwa tayari kukabiliana na hali ile. Watoto nao walianza kulia kwani nao hawakuamini kilichokuwa kinaendelea kwenye maisha yao kwa wakati ule.

Haikuwa rahisi kuamini. Majirani zao waliamua kuwahifadhi kwa muda kwa kuwa ilikuwa tayari ni usiku. Asubuhi kulipopambazuka, yule mwanamke tayari alikuwa kichaa, akivua nguo na kuokota makopo barabarani.

Majirani kwa kushirikiana na ndugu zake yule mama walimrudisha kijijini kwao Urambo, Tabora ili ahudumiwe huko kutokana na kukosa msaada na ushirikiano toka kwa mumewe waliyedai hakuwapo nyumbani. Watoto pia iliwalazimu waende kijijini na mama yao kwani hawakuwa na mwelekeo.

Hali ile iliendelea kwa miezi mitano hadi alipopelekwa kwenye kanisa la watu waliookoka kuombewa huko kijijini. Baada ya kuwa amefunguliwa kupitia maombi, alipewa shilingi 50,000 kama msaada wa chakula.

Hata hivyo, baada ya kupatiwa fedha hizo hakununua chakula bali aliwaza nini afanye ili aendeleze maisha yake. Alikuja kugundua kuwa mumewe alikuwa hamtaki tena. Aliamua kununua khanga za bei ya jumla na kuanza kuuza rejareja kwenye nyumba za watu kama machinga pale kijijini kwao.

Mpenzi msomaji, unaishi na mwenzio lakini hujui nini anachokuwazia. Huo ndio ulimwengu wa roho usioonekana kwa macho.

Je, unajua nini kilichoendelea kati ya wanandoa hawa wawili? Nani aliyekuja kuaibika au kuharibikiwa mwishoni? Ubabe wa baba yule ulikuwa wa faida kwake au hasara?

***Fuatilia sehemu ya pili ya makala haya wiki ijayo. Pia kama unayo maoni, ushauri au kisa cha kimaisha tuma ujumbe mfupi kupitia 0715208581. Namba hii pia ipo WhatsAPP.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Bei kipimo COVID-19 maumivu kwa watu wa chini

HIVI karibuni serikali ilitangaza kupanda kwa bei ya kupima virusi vya homa kali ya mapafu (corona) kutoka Sh. 58,000 kwa Mtanzania ambayo ilikuwa Sh. 18,000 ya kulipa hospitali unakopatia huduma na Sh. 40,000 ya Maabara Kuu ya Taifa.

Bei hiyo ilipanda hadi kufikia Sh. 230,000 yaani Dola 100 ambazo awali zililipwa na raia wa kigeni waliopima ili kupata cheti maalum kwa ajili ya kuvuka mpaka.

Uamuzi huu umekuja katika kipindi ambacho huwezi kuvuka mpaka wowote wa nchi bila kupima virusi hivyo na kupata cheti maalum na unaporudi nchini unatakiwa pia kupima ndipo uvuke mpaka husika na kote ni gharama.

Sina ubishi na kupanda kwa gharama hizo lakini nimejaribu kufikiri juu ya mfanyabiashara wa kawaida ambaye huenda nchi za Uganda na kwingine kufunga mzigo kwamba kwa sasa katika gharama zake ni lazima awe na Sh. 230,000 ili apime na kupata cheti.

Lakini pia nimejaribu kwafikiria madereva wa magari yaendayo Zambia, Kenya, Malawi, Uganda na Msumbuji kwamba ni kwa kiasi gani sasa watakuwa na gharama kubwa ya kupima wanapotoka nchini na kurudi nchini.

Serikali imetangaza kuwa Tanzania hakuna corona lakini msisitizo mkubwa ni wananchi kuchukua tahadhari muhimu kama kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka mikusanyiko na hatua nyinginezo za kujikinga kwa kuwa bado mipaka yetu inaruhusu watu kuingia na kutoka.

Nimewaza kwa sauti ni kwa kiasi gani wafanyabiashara waliokuwa wanakwenda Uganda kufunga mzigo wanashindwa kufanya hivyo na wanapojaribu kuagiza wanaishia kutapeliwa.

Lakini kundi lingine ni madereva wa mabasi ya nje ya nchi ambao lazima wasafiri na wapime kwamba kama kwa mwezi ana safari mbili, basi ni lazima apime mara mbili na kutumia Sh. 460,000.

Na kama kila mwezi anasafiri mara moja maana yake ni lazima awe na kiasi hicho cha fedha na zaidi hasa kutegemea na nchi anayokwenda inapima corona kwa kiasi gani cha fedha. Maana yake tajiri atalazimika kubeba gharama hizo na moja kwa moja hatazibeba yeye bali zitabebwa na wananchi kwa kuwa lazima bei ya bidhaa itaongezeka.

Ni muhimu sana makundi haya yakafikiriwa na kupewa huruma kwa kuwa wako ambao wanasafiri kwa ajili ya kuhudhuria mikutano na vikao mbalimbali ambavyo hugharamiwa lakini wapo ambao ni lazima wasafiri kwa sababu za kibiashara.

Wapo pia wengine ambao ndugu zao wanaishi nchi jirani na mara kwa mra hutembeleana. Mathalani, wako Watanzania wengi wanaoishi Mombasa na kuna usafiri wa moja kwa moja kwenda huko na wengi ni wale wa kipato cha chini ambao hawawezi kumudu kiasi hicho cha fedha.

Nimewaza kwamba watu hawa wanataka kurudi nchini au kwenda kuona familia zao na wanauwezo wa nauli pekee, na wako watatu au wanne maana yake si chini ya Sh. milioni moja kupata huduma hiyo, jambo ambalo ni muhimu likaangaliwa kwa jicho la pekee.

Pamoja na kwamba imeonekana ni muhimu kupanda kwa gharama hizi, ni muhimu sana kuangalia sababu za wanaotakiwa kupima na kugawa na makundi yenye gharama tofauti katika kupima kipimo hicho.

Tunajua watu wengi wa mipakani na ukanda wa Pwani kuna miezi kadhaa huishi nchini na mingine huishi nchi jirani ambako familia zao ziko huko. Je, mtu huyu atawezaje kuendelea kuona wapendwa wake ikiwa gharama za kupima ni kubwa kiasi hiki?

Nawaza kuwa ni muhimu sana kwa jambo hili kuangaliwa kwa jicho la pekee ili kuwawezesha kuendelea na shughuli zao za kila siku, kutembeleana na kuzikana. Kwa kufanya hivyo, wafanyabiashara wataendelea na kazi zao ambazo kwa kiasi kikubwa zitachangia pato binafsi na pato la taifa kwa ujumla.

***Mungu Ibariki Tanzania***

# KIPAIMARA









Ilikuwa furaha kwa familia ya Shama, baada ya binti yao Alicia Amos kupata kipaimara katika kanisa za Kiinjili la Kilutheri la Korogwe Desemba 26, mwaka jana.





# MITINDO



## UKIVAA HIVI utafanya chaguo sahihi

MAVAZI ni moja ya pambo linalomfanya mtu kuwa na mwonekano tofauti.

Mara nyingi uchaguzi wa mavazi unasababisha kmuhusika kupendeza kama akichagua vizuri au kuchukiza edapo hatakuwa na chaguo sahihi.

Kwa kawaida wanaume hawajali sana kuchagua nguo za kuvaa kulingana na hitaji la mwili wake, badala yake wanavaa baada ya kuona kwa mtu, shinikizo kutoka rafiki yake wa karibu au pale mtindo mpya unapoingia.

Kutokana na sababu hizo, mtu anajikijuta nguo anayovaa hailingani umbo na rangi yake ya mwili. Kama unataka kufanya chaguo sahihi la nguo zako, chukua hatua zifuatazo.

### CHAGUA RANGI YA NGUO

Kwa kawaida nguo nyeusi haichagui rangi ya ngozi ya mtu, mwanamume anapovaa suruali yeusi haitaji kufikiri sana kuhusu rangi ya shati atakalovaa.

Unapovaa Suruali nyeusi, hakikisha unavaa shati au fulana ya rangi yoyote yenye mng'aro itakutoa bomba.

Kwa shati au fulana nyeusi inaedana vizuri na suruali ya jeans, nyeupe au rangi yoyote nayopenda.

### USIVAE NGUO NYINGI

Watu wengine wana kawaida ya kuvaa nguo nyingi kwa wakati mmoja, tabia hii inasababisha muhusika kuwa na umbo lisiloeleweka na kusababisha kupoteza muonekano wake.

Hakikisha unavaa nguo zinazoweza kukupatia nafasi ya kutembea bila shida na mwili wako kufanya kazi bila usumufu.

### HALI YAHEWA

Wengu hawajui namna ya kuvaa nguo kulingana na hali ya hewa, unatakiwa kuwa makini na jambo hilo ili kujiepusha na usumbufu.

Wakati wa joto, unatakiwa kuvaa nguo zinazoruhusu mwili kupumua, hivyo usivae nguo nzito zinzovaliwa kipindi cha baridi kwa ajili ya kukupa uhuru wa kutembea.



## UREMBO





### UWEKAJI ‘WEAVING’

# Urembo unaosumbua wanawake wengi

UREMBO wa mwanamke hujitambulisha kutokana na muonekano wake kulingana na namna anavyojiweka katika maisha yake ya kila siku.

Kujiweka vizuri kuanzia nguo, usafi wa mwili na kila kitu kinachomzunguka. Leo tutazungumzia urembo wa ushonaji wa nywele bandia maarufu kama ‘weaving’ na utunzaji wake.

Urembo huu kwa wanawake kwa namna moja hawawezi kuepukana nao kutokana na ufanisi wake katika kupendezesha muhusika.

Ushonaji wa nywele bandia husaidia wanawake wengi hasa wale wenye nywele fupi na pia wenye nywele chache kuonekana na mvuto wa kipekee.

Pia kwa wanawake wenye nywele ndefu huwapa chaguo la kuonekana tofauti. Pamoja na kwamba aina hii imekuwa inasaidia kwa kiasi fulani, lakini baadhi ya wanawake wanashindwa kuzitunza vizuri nywele baada ya kushonea au namna ya kuchagua rangi zinazoendana na ngozi zao.

Lakini pia wamekuwa wakikosea katika ushonaji wake jambo ambalo wakati mwingine wanaonekana kituko.

#### UTUNZAJI WAKE

Nataka kuwakumbusha kuwa ‘weave’ inatakiwa kutunza vizuri ili kutosababisha kero kwa wengine kutokana na harufu kali inayotokana na kuganda kwa jasho.

Unatakiwa kuhakikisha nywele zako zinashonwa na wataalam anayefahamu namna ya kushona kulingana na sura ya mtu husika.

Ili nywele siwe safi, ni muhimu kabla ya kushona uoshe nywele zako za asili. Usikubali kuweka nywele bandia kabla ya kuosha kwa sababu uchafu wa ndani wa nywele za asili unaweza kusababisha uvundo.

Baada ya kuosha na kushona hakikisha unapata mafuta ya kujipaka ili ywele zionekane zenye mng`ao mzuri.

#### KILEMBA HATARI

Epuka kufunga kilemba kizito na kisicho na matundu ya kupitisha hewa kwa kipindi kirefu kwa sababu kitatengeneza jasho ndani na hivyo kufanya nywele kutoa harufu.

Itakuwa ni vema kama hautakaa na nywele bandia kwa kipindi kirefu, kwani itakusaidia kutumia tena baadae.

## MAPISHI

### Na Mary Geofrey

# Namna ya kupika makaroni



CHAKULA cha makaroni kina njia mbalimbali rahisi za kuandaa, hivyo chakula hiki ni kizuri na chenye kujenga afya.

#### MAHITAJI

Makaroni nusu pakiti, pima kutokana na mahitaji yako, nyanya nne zilizoiva vizuri, nyanya ya kopovijiko 3, vitunguu maji viwili na kitunguu saumu kimoja.

Pilipili hoho moja, soya sauce kijiko kimoja, chumvi kijiko kimoja, giligilani kijiko kimoja kikubwa, masala kijiko kidogo kimoja na unga wa Curry.

Pia tangawizi nusu kijiko kidogo, nazi moja njegere glasi moja, bilinganya moja, pilipili ndefu mbili kata vipande vidogo vidogo na ‘Cayenne pepper’ kijiko kidogo kimoja.

#### MAELEKEZO

Unaweza kuongeza viungo unavyopendelea ili kukifanya chakula kiwe kitamu.

Ila kama unakula na watoto, hakikisha unapunguza wingi wa pilipili, maana watoto hawataweza kuhimili ukali wake.

Andaa viungo, menya nyanya, vitunguu maji 2, pilipili hoho na kitunguu saumu. Kata vipande vidogo, hifadhi pembeni. Kamua tui zito la nazi, hifadhi pembeni.

Andaa njegere, zichemshe. Ila zisiive sana, epua na weka pembeni.

Kwenye sufuria, weka maji na chumvi, acha yachemke. Weka makaroni, pika kwa dakika 7 hadi 8 (fuata muda elekezi kwenye paketi ya makaroni) kisha epua na chuja maji, hifadhi pembeni.

Ni vizuri ukipika makaroni dakika 1 au 2 chini ya muda elekezi kwenye paketi, hii itafanya makaroni yaive vizuri yakichanganywa na sauce na wakati wa kumalizia kupika.







Weka mafuta ya kula kwenye sufuria, bandika jikoni. Acha mafuta yapate moto vizuri kisha weka kitunguu maji. Pika kwa dakika mbili huku unakoroga. Weka kitunguu saumu, curry powder, tangawizi, pilipili ndefu, giligilani ya unga, italian season na gharam masala. Halafu koroga vizuri kisha weka nyanya. Koroga vizuri kisha acha ziive hadi zitengane na mafuta.

Weka nyanya ya kopo na bilinganya, koroga pamoja.

Weka njegere, koroga pamoja, soy sauce pamoja na chumvi kiasi na makaroni kwenye sufuria. Changanya na sauce ya nyanya na njegere, weka pilipili hoho, koroga na acha ziive kiasi, ili harufu iwe tamu na nzuri.

Weka tui la nazi, geuza mara kwa mara kisha acha chakula kichemke kidogo na nyunyizia cayenne pepper na pilipili manga ichanganye na chakula kisha epua.

Chakula kitakuwa tayari ili upate ladha zaidi, kula chakula hiki kikiwa bado cha moto.

Mapishi haya ni kwa msaada wa blog ya misosi.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Umuhimu wa umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba



KATIKA nyumba leo tunazungumzia umuhimu wa kuzingatia umaliziaji mzuri wa dari.

Hii ni sehemu ambayo watu wengi wanaojenga nyumba zao husahau kuipa kipaumbele, lakini Msanifu wa nyumba, Kimboi Marick, anasema hiyo ni sehemu muhimu zaidi kwa sababu ndio hupendezesha zaidi nyumba.

Marick anasema dari katika ujenzi wa nyumba mara nyingi watu wengi hawaipi angalizo kubwa, lakini ni sehemu ambayo endapo isipomaliziwa vizuri inaweza kuharibu kazi yote nzuri ya ujenzi.

Pia, anasema kwa sababu inaficha vitu vingi kwa ndani, isipojengwa au kumaliziwa vizuri kitalaam inaweza kuleta athari kubwa kwenye nyumba.

"Dari imekuwa ni sehemu ambayo inasahaulika sana katika ujenzi wa nyumba zetu, kwa maana ya kuwa inapewa angalizo kidogo sana, lakini umaliziaji mzuri wa dari hili ndio unaozidisha uzuri wa nyumba yako, inasaidia kuiweka imara na kwa usalama zaidi," anasema Marick.

"Dari ndilo linaficha bomba za umeme na huduma nyingine ikiwamo kuondoa uzia kwenye macho ya watu wanaoingia au kuishi kwenye nyumba husika na kuipa muonekano mzuri. Ili upate faida zote za dari hili ni vyema kumpata fundi au msanifu mzuri wa majengo anayeweza kusimamia kazi hiyo kwa ufanisi unaotakiwa."

Anasema kabla ya kufanya uamuzi wa umaliziaji wa nyumba yako ni vyema ujitafakari na kufanya uamuzi kwanza wa aina ya muonekano wa dari unalolitaka kwenye nyumba yako ili kuepuka kujilaumu baadaye.

"Tafakari na uamue, unataka kupata muonekano gani, fanya uamuzi sahihi ni muundo gani wa dari unalolihitaji, usikurupuke ili ukajilaumu baadaye, kumbuka kuna dari linalotakiwa kutengenezwa sebuleni, vyumbani, jikoni na hata vyooni. Na katika kila maeneo yote hayo unatakiwa kuamua."

"Unaweza kuamua muonekano wa dari la sebuleni ukawa tofauti na wa vyumbani au ukafanana, hiyo yote itategemea na namna unavyopendelea wewe, lakini la muhimu kuzingatia ni kwamba unatakiwa kuhakikisha unatumia watu ambao ni wataalamu ili walimalizie vizuri na kuiweka nyumba katika hali ya usalama zaidi."

## MPANGILIO

## Dondoo ya kuweka televisheni ukutani katika sebule yako

**1:** Weka Runinga yako chini kwa uangalifu mkubwa au kwenye kochi ili isivunjike.

**2:** Chukua henga ya tv ya ukutani na upime kisha toboa katika zile alama ulizoziweka kwa kutumia drili maana inatakiwa hali ya usafi.


**3:** Angalia nyuma ya tv yako kuna sukurubu nne, fungua na uweke ile vyumba vya henga na ufunge kwa umakini.

**4:** Baada ya hapo, funga henga ukutani, na hakikisha unakaza vizuri ili kuepusha kuanguka.

5: Ingiza nyaya zako kuanzia juu kuja chini katika mtiririko maalum na hapo funga Tv yako kwa ajili ya kuburudika.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MTEULE
KIYOYOZI PULIZA "MAKABLASHA" MIMI NAKIMBIZANA NA KERO JUANI...
TUKIFIKA BAR, ILI TUSICHANGANYANE ANZA KUAGIZA, ALAFU TUKISHALEWA NAAGIZA MIMI KWA FUJO.
EMBU WEKA VIZURI SENTESI YAKO NAHISI KUNA SIASA HAPO INAINGIA....
ONESHA HELA
UMESIMAMA UMEJIKUNYATA BILA KUSEMA CHOCHOTE! TUKUSAIDIE NINI?
'MNA BUKU?
SHIKAMOO POMBE KALI, SIJAWAHI KUSIKIA HARUFU YA MAINI YANGU YAKIUNGUA! LEO NDO RASMI
AIYAAAAAAH! KUMBE SIKU NILIYOLEWA NILI-KWENDA UKWENI KUOMBA KAZI!
UMEOMBA ETI UWE 'NESI' ...KWA HIYO CHUMBA CHA WAKWE ZAKO NI WODI?
DUH! KUMBE MAISHA YANA-CHENJI" JAPO HAYANA MFUKO!
MZEE MWENZANGU MAMBO YAMETAITI KAMA SURUALI ZA VIJANA WA KISASA!
AAAAAAAAH!!! HAKUNA CHA TAITI WALA MODO...NIPE KODI YANGU!
VIBINTI HAVINITAKI KISA MZEE... KILA NIKI-FURUKUTA NAJIBIWA HIVYO!
TUNATIBU MAPENZI'
MIMI MWENYEWE NIMETOKA KUJIBIWA MUDA SI MREFU!..
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MACHO YANAPONZA MWILI...

## HABARI KIMATAIFA



Mke wa Rais wa Marekani, Dk. Jill Biden, akizungumza na wanajeshi waliokuwa wakilinda jengo la bunge la nchi hiyo Capital Hill baada ya kusambaa picha wakiwa wamelala katika maegesho ya magari **(PICHA: AP)**

# Biden aomba msamaha wanajeshi kulala nje

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden , ameomba msamaha baada ya baadhi ya wanajeshi waliokuwa wamewekwa kulinda eneo la Capitol Hill kupigwa picha wakiwa wamelala katika eneo la kuegesha magari.

Zaidi ya wanajeshi 25,000 walipelekwa Washington DC kwa ajili ya kulinda amani wakati wa kuapishwa kwake Januari 20.

Picha zilizopigwa wanajeshi hao zilianza kusambaa mtandaoni siku ya Alhamisi, zikiwaonyesha wakiwa wamelala eneo la kuegesha magari ya wabunge.

Hali hiyo ilisababisha hasira miongoni mwa wanasiasa, huku baadhi ya magavana wakiamua kuwaondoa wanajeshi wao kutokana na utata huo.

Rais Biden alizungumza na mkuu wa jeshi la kulinda usalama wa taifa, kuomba msamaha na kuuliza hatua gani iliyotakiwa kuchukuliwa kuweka mambo sawa.

Mke wa Rais huyo, Jill Biden, alitembelea baadhi ya vikosi hivyo kwa ajili ya kuwashukuru akiwa amewabebea biskuti kutoka Ikulu kama zawadi.

"Leo hii nilitaka tu kuja na kuwashukuru kwa kutulinda mimi pamoja na familia yangu," alisema.

Hata hivyo, mke wa kiongozi huyo aliwatembelea baadhi ya wanajeshi waliopata tatizo hilo.

Kuna taarifa za kukanganya kuhusu kwanini wanajeshi hao walipelekwa Capitol Hill, lakini waliviambia vyombo vya habari kwamba agizo hilo liliwafikia siku ya Alhamisi mchana bila maelezo yoyote.

Ofisa mmoja wa Marekani ambaye hakutaka kujulikana, aliliambia shirika la habari la Reuters, kuwa kati ya wanajeshi 100 na 200 ya waliopelekwa eneo hilo walikuwa na virusi vya corona.

Baada ya picha hizo kuanza kusambaa, wabunge walionyesha kukerwa na wengine waliamua kitoa ofisi zao kama kwa wanajeshi hao kwa ajili ya kupumzika.

Hata hivyo, wanajeshi hao waliruhusiwa baada ya uamuzi wa kulinda eneo hilo kutenguliwa.

Gavana wa jimbo la Florida, Ron DeSantis, alikuwa miongoni mwa wale waliosema kuwa ametoa agizo wanajeshi wa jimbo lake kurejea nyumbani kufuatia mtafaruku huo.

Chuck Schumer, Mbunge wa Democrat na kiongozi mpya wa Bunge la Seneti, alisema kilichotokea ni jambo baya na aliahidi halitarejea tena.

**BBC**

# Waandamanaji 200 wakamatwa Urusi

**MOSCOW, Urusi**

ZAIDI ya waandamanaji 200 wamekamatwa na polisi nchini Urusi wakati maandamano ya kumuunga mkono mwanasiasa wa upinzani Alexei Navalny, ambaye amefungwa jela baada ya kurudi nchini humo.

Kiongozi huyo wa upinzani aliitisha maandamano makubwa mara baada ya kukamatwa na kupelekwa jela wakati aliporejea nchini humo kutoka Ujerumani ambako alikuwa akipatiwa matibabu baada ya kunusurika jaribio la kulishwa sumu ya Novichok.

Alikamatwa katika uwanja wa ndege wa Sheremetyevo na kufungwa.

Katika kuhamasisha maandamano hayo, timu ya mwanasiasa huyo wa upinzani ilitoa nyaraka za uchunguzi kuhusiana na mali za kifahari anazomiliki Putin zilizopo katika bahari nyeusi.

Katika bandari ya Vladivostok waandamanaji walikusanyika katikati ya mji huo, wakipaza sauti za kutaka Navalny kuachiwa huru.

Waandamanaji wengine walikusanyika katika miji ya mashariki ya mbali na Mkoa wa Siberia ikiwamo Khabarovsk, Novosibirsk na Chita.

Shirika moja ambalo linafuatilia mikutano ya upinzani limesema kwa kukadiria polisi wamewakamata watu zaidi ya 200 kwenye miji 20.

# Wanamgambo 189 wa Al Shabab wauawa

**MOGADISHU, Somalia**

WANAJESHI wa Uganda wanaounda kikosi cha kimataifa cha kulinda amani nchini Somalia, wamewaua wapiganaji 189 wa kundi la al-Shabaab lenye mafungamano na mtandao wa kigaidi wa al-Qaeda.

Taarifa ya Jeshi la Ulinzi la Uganda (UPDF) ilisema tukio hilo lilitokea juzi baada ya wanajeshi wake kuvamia maficho ya al-Shabaab katika vijiji vya Sigaale, Adimole na Kayitoy, kusini magharibi mwa mji mkuu Mogadishu.

Katika tukio hilo viliharibiwa vifaa vya kijeshi na vifaa vinavyotumiwa katika mashambulizi ya kigaidi.

Hata hivyo, hakuna kauli yoyote kutoka kundi hilo kuhusu shambulizi hilo.

**DW.**

# Zimbabwe yatangaza kukabiliana na Corona

**HARARE, Zimbabwe**

ZIMBABWE imetangaza mipango ya kuimarisha udhibiti wa usambaaji wa ugonjwa wa Covid-19, baada ya mawaziri wawili kufariki dunia kwa muda wa siku chache.

Mawaziri ambao walifariki kwa muda wa siku mbili ni Waziri wa Uchukuzi Joel Matiza na Waziri wa Mambo ya Kigeni, Sibusiso Moyo, ambao wote walipata maambukizi ya virusi vya corona.

Mpaka sasa mawaziri wanne wa serikali wamefariki kutokana na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari, mawaziri kadhaa wa serikali wako katika hali mbaya kwenye hospitali moja ya binafsi.

Hadi jana nchi hiyo ilisajili visa 30,523 vya maambukizi ya corona ma vifo 962 tangu kuanza kwa ugonjwa huo.

**DW.**

SAFU

# Ushiriki hafifu wa wananchi katika shughuli za maendeleo



Na Magabilo Masambu

MAENDELEO katika nchi huletwa na wananchi mwenyewe. Kwa hiyo ushirikiano baina ya wananchi kwa wananchi au wananchi na viongozi ni jambo muhimu katika kujiletea maendeleo.

Pamoja na ukweli kwamba wananchi ndio wajenga nchi, wanapaswa kushiriki katika ujenzi huo, wakiona fahari ya kufanya hivyo na kwamba wao ndiyo wanaostahili kuijenga nchi yao hakuna mwingine. Siku tukifikia kiwango hicho cha fikra, maendeleo ya nchi yetu yatapaa wakati kila mmoja ndani ya nchi akiwa na furaha.

Miaka ya hivi karibuni, ushiriki wa wananchi katika shughuli za ujenzi wa taifa zimeanza kuonekana kama ni adhabu. Ni kweli kwamba hata zamani miaka ile ya kodi za kichwa, kuna baadhi ya wananchi ilikuwa lazima kuwalazimisha watoe kodi hizo lakini pia katika shughuli nyinginezo. Naanza kuona hali hiyo ikianza kujirudia.

Nafikiri tunaweza kukubaliana kwamba tatizo lipo. Tukijidanganya kwamba halipo basi hatutapata njia ya kulitatua isipokuwa tutakuwa tumelitatua kwa kujifanya kwamba hakuna tatizo. Viongozi wa ngazi za chini wanaweza kuthibitisha hili wanavyohangaika na wananchi katika shughuli za maendeleo. Mfano katika ujenzi wa shule, vituo vya afya na kadhalika.

Sasa kuna mambo yakifanyika yanaweza kuwafanya wananchi waonekane hawataki kushiriki katika shughuli zinazowahusu kimaendeleo na yakirekebishwa wananchi watakuwa na hali ya kushiriki katika shughuli hizo bila kusukumwa, japo wanaohitaji kusukumwa hawatakosekana lakini kwa kiwango kidogo.

Moja, kwa maoni yangu tatizo huwa linaanzia kwenye kampeni za uchaguzi. Wagombea wa ngazi mbalimbali mnapokutana na wapigakura mnawaaminisha kwamba kila kitu mtafanya nyie. Utasikia mgombea akijinadi mkinichagua nitawajengea hiki, nitawafanyia kile na kadhalika. Kwa hiyo wananchi wanakuchagua wakiamini kila ulichokiahidi utakileta.

Ukishachaguliwa unagundua kwamba ulivyoahidi haviwezekani na hivyo kurudi kwao kuwaambia tunataka mchango huu na ule ili tujenge hiki na kile. Kumbe wakati wa kampeni unapaswa kuwaambia nini basi? Unasema nichagueni ili nikishinda tushirikiane pamoja kufanya kadha wa kadha, hivyo litakuwa jambo la kawaida utakapokuja kwao kuwaambia unahitaji mchango au nguvu zao katika jambo fulani maana hukuahidi kuleta chochote bali kushirikiana nao.

Pili, uwazi katika michango yao. Uwazi juu ya matumizi ya michango inayotoka kwa wananchi ni muhimu katika kujenga uaminifu. Kama michango imetolewa kwa ajili ya choo lakini baadaye viongozi mkagundua kwamba choo si muhimu zaidi kuliko darasa, ni lazima mrudi kwa wananchi kuwaeleza kwanini mnataka kujenga darasa badala ya choo sio mnakaa kwenye vikao vyenu mnaamua tu. Inawezekana pesa kweli haijaliwa na mmefanya jambo jema lakini hiyo haitoshi taarifa kwa watoa pesa ni muhimu sana kuondoa sintofahamu.

Tatu, ni juu ya kipato. Hali ya maisha si nzuri lakini hatuwezi kuacha kushiriki kwenye maendeleo yetu kwasababu ya ukosefu wa fedha. Fedha ni matokeo ya juhudi zenye maarifa katika kujiletea maendeleo lakini si kila kitu kinahitaji fedha.

Kama fedha ni tatizo wananchi wapewe uhuru wa nini wanaweza kutoa kwa ajili ya maendelo. Namaanisha vitu mbadala wa fedha vinaweza kutumika mfano kama mwananchi hana pesa, anaweza kutoa mazao, mifugo na kadhalika kisha vitu hivyo vibadilishwe kuwa fedha kwa kuviuza.

Wakati wa vita vya Kagera, wananchi hawakuwa na fedha za kuchangia, hivyo wengine walichangia mifugo na chakula. Tusielekeze mawazo yetu kwenye fedha tu, washirikishwe waone namna bora ya kushiriki hata kutoa nguvu zao. Wengine wangependa kufyatua tofali, kuleta mawe, wengine ni mafundi wangependa kujitolea kujenga.

Nne, ushawishi wa viongozi. Sifa ya kwanza kabisa ya kiongozi ni kuwa na uwezo mkubwa wa kushawishi. Kiongozi akikosa sifa hiyo, hugeuka na kuwa mtawala. Uwezo wa kushawishi hausomewi japo unaweza kujifunza njia za kutumia, lakini kwa kiasi kikubwa ni karama.

Kiongozi akikosa sifa ya ushawishi kwa wananchi atakuwa na wakati mgumu sana katika kuhamasisha shughuli za maendeleo itafika mahali anaona njia rahisi ni kupiga jambo ambalo halikubaliki Kisheria.

Wakati wa uchaguzi ni muhimu sana wananchi kujipatia viongozi wanaowataka. Itakuwa rahisi kushirikiana nao katika shughuli za maendeleo. Hizi ni baadhi tu ya sababu ambazo zinaweza kusababisha wananchi kuwa na ushiriki hafifu katika maendeleo yao.

Kinyume chake hatu za makusudi zikichukuliwa ikiwa ni pamoja na elimu zaidi kuhusu athari za kutoshiriki kwa maisha yao ya baadaye. Naamini wananchi watajitolea kujenga nchi yao. Wakati mwingine tusiwalaumu tu tutafute wapi tatizo lilipo.

# Hata watoto watundu walitulia kipindi cha 'Mama na Mwana'



Na Adam Fungamwango

WIKI mbili zilizopita tulikuwa na mada ya wanafunzi wa katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1990 kukichukia kipindi cha 'Kumekucha' na wimbo wake ambao jina lake linafanana na kipindi.

Kisa ni kwamba tu ndiyo kipindi ambacho kilikuwa kikianza wakati wanafunzi wanatakiwa kuamka na kuwahi kwenda shuleni. Kutokana na mazingira na wakati uliopo, walijikuta wakikichukia kipindi hicho.

Kwanza muda huo wakati wimbo huo unasikika walikuwa wanatakiwa waamke na kujiandaa kwenda shuleni. Halafu wakati wimbo huo unamalizika, wanatakiwa wawe wameshafika shuleni na kupata namba. Vinginevyo bakora zinawahusu.

Leo tuko tofauti kidogo. Tunaangalia kipindi ambacho kilikuwa kipenzi cha wanafunzi na watoto enzi hizo. Hiki ni kipindi cha 'Mama na Mwana.' Ni kipindi kilichopendwa mno na watoto pamoja na wanafunzi.

Hiyo ni kutokana na maudhui ya kipindi chenyewe, watoto wanaofanana na umri wao pamoja na mambo ya shule.

Ni kipindi kilichokuwa maarufu sana miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990. Kilikuwa kikiendeshwa na watangazaji wa kike, ambao walikifanya kipendwe mno kutokana na jinsi wanavyotangaza, maana walijua kabisa wanaowatangazia si wakubwa wenzao, bali ni watoto ambao bado hawajaanza shule na wanaosoma.

Lugha iliyotumika ni kama ile ya mama na mtoto wake, au bibi na mjukuu wake. Mtangazaji wa kwanza kabisa ambao hawezi kusahaulika na watoto au wanafunzi wa wakati ule ni Debora Mwenda. Mama huyu kwa kweli alikifanya kipindi cha 'Mama na Mwana' kuwa bora ambacho hakuna mtoto aliyetaka kukikosa.

Kilikuwa kikianza Jumamosi mchana, siku ambayo watoto hawaendi shuleni, lakini kilirudiwa Jumapili jioni. Muda ambao kipindi kinakaribia kuanza, watoto wanakula mapema na kukisubiri. Kikianza kila mmoja anataka kuwa karibu na redio ili wasikilize nini kimeandaliwa siku hiyo.

Kwenye kipindi hicho hawakupita watangazaji wengi, nadhani Radio Tanzania Dar es Salaam, walikuwa wanataka wale tu ambao wana uwezo wa kuzungumza na hadhira ya watoto huko majumbani. Mtangazaji mwingine ambaye naye atakumbukwa kuwa aliweza kukonga nyoyo za watoto ni Sarah Dumba.

Tukija kwenye kipindi chenyewe, pamoja na mambo ya shule kama vile masomo, kwaya, na vingine vinavyofanana na hivyo, kubwa watoto walipenda mno hadithi. Ubunifu wa RTD na Debora mwenyewe hadithi zilivyokuwa zikisimuliwa, ndiyo ulisababisha hata wakubwa nao kupenda kipindi hicho.

Hakukuwa na televisheni kipindi hicho, lakini usimuliaji wake, ulifanywa kwa namna ya maigizo hivi. Yaani kama kuna zimwi, basi ilirekodiwa sauti fulani hivi ikaongezwa na utaalam wa teknolojia ya wakati huo, basi ikaonekana sauti moja nene, nzito, yenye mikwaruzo na yenye kutisha.

Malki alikuwa na sauti yake, mfalme naye alikuwa na sauti yake, ili mradi hadithi zake zilikuwa kama tamthilia, maigizo au filamu.

Watangazaji kama Charles Hillary, Sekioni Kitojo, Michael Katembo, Nadhir Mayoka na wengineo kwa kiasi kikubwa walitumika sana kuingiza sauti za kuigiza kwenye hadithi hizo. Mfano Charles aliigiza kama mfanyabishara kwenye hadithi ya 'Ua Jekundu', Mayoka aliigiza kama 'Kamal' kwenye hadithi ya 'Siri binti Mfalme'.

Ilikuwa burudani ya aina yake, kwani kila mmoja alikuwa akivuta taswira yake jinsi anavyoisikia hadithi. Kumbuka kuwa wakati huo kwa Tanzania Bara, televisheni ilikuwa ni ndoto ya mchana, hivyo kila mmoja alijitahidi kujiwekea televisheni yake kichwani, kuona mfanyabiashra anafananaje, na hata jitu la msituni linafananaje.

Hadithi zilizopendwa sana wakati ule ni kama hizi zilizotangulia kuzitaja 'Ua Jekundu', watoto walita jitu la msituni, 'Siri Binti Mfalme' hadithi iliyotoka kwenye kitabu cha Alfu Lela Ulela iitwayo Kamaralzaman na Badoura binti mfalme, 'Mbalamwezi Nyota Begani', 'Jadi Mbaharia' iliyosimuliwa kutoka kwenye hadithi ya 'Sindbad Baharia', 'Binti Chura' na zingine nyingi.

Hata hivyo, hadithi ambazo kila mmoja hawezi kuzisahau kwanza kabisa ni ile ya mfanyabiashara anakwenda safari ya mbali na mabinti zake kila mmoja kuagiza zawadi, lakini wa mwisho akaagiza ua jekundu. Baba huyo alifika kwenye jumba kubwa la ajabu lililokuwa lina kila kitu.

Kwenye bustani alikutana na ua jekundu alipolichuma, lilitokea jitu kubwa lenye hasira lililotaka kumrarua, lakini mwisho ya siku lilimuachia kwa masharti ya kumruhusu binti yake mmoja kati ya watatu aje kuishi naye pale. Baba aliporudi nyumbani, binti yule yule mdogo alikubali kwenda kuishi.

Mwisho wa hadithi ilikuwa jitu lile zamani alikuwa ni Mwanamfalme aliretupiwa uchawi na masharti yake ili apone ilikuwa ni kuliliwa machozi na binadamu. Kumbuka binti yule alipata ruhusa kwenda kwao, akachelewa kurudi aliporejea alilikuta jitu limekufa, binti akalia sana na machozi yakamdondokea, uchawi ukaondoka na kugeuka kijana mzuri. Wakafunga ndoa.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilimfanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.

Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Wazo la kumpigia moja kwa moja na kumwaarifu jambo lile nalo hakukubaliana nalo.

Ni kwamba huenda mumewe angekuwepo. Halafu angemwambia, wangefanikisha hayo yote mtoto akapatikana.

Lakini baadaye, mwanamume ni mwanamume tu, siku isiyo na jina mumewe anaweza akamuuliza, yule alikuwa nani? Na kwa nini aliamua kufanya kazi hii yote ya hatari? Nia ilikuwa nini kutoa msaada huo wote? Na mlikutana naye wapi? Mnajuana naye vipi?.

Hilo ndilo lilimtisha na kumfanya asite kumpiga simu ya moja kwa moja.

Akakumbuka tukio moja ambalo jamaa alifungwa jela miaka 10, lakini mkewe anapigana kufa na kupona kuhakikisha mumewe anatoka. Akatembea na ofisa mmoja mkubwa wa Magereza ambaye alimrubuni na kumwambia akifanya hivyo, mumewe atatoka. Na kweli ikawa hivyo. Mke hakumwambia mumewe. Ikawa siri.

Lakini duniani hakuna siri ya watu wawili, mume akajua. Badala ya kufurahi kuwa mkewe amefanya mbinu yeye ametoka kwenye kifungo ambacho angekaa ndani miaka 10, badala yake akakaa miezi minne tu, akampiga mkewe na kumsemea maneno ya dhihaka.

Ingawa ndoa iliendelea, ilimuumiza sana mume. Hiyo ndiyo tabia ya wanaume.

Ndiyo maana alihofia. Alichoona kwanza kinachoweza kumsaidia ni kutuma meseji ya salaam. Ikajibiwa baada ya dakika tano. Akauliza kama mumewe yupo. Akajibiwa ametoka kidogo. Akampigia.

Baada ya salamu, Neema alitiririka jinsi alivyoporwa mtoto na sasa ana wiki zima yuko nyumbani. Jerry hakumwambia chochote juu ya alichokiona, badala yake akamtaka waonane.

"Naomba ukiwa na nafasi kesho au keshokutwa tukutane, tuongee."

"Nini tena Jerry?"


"Hilo suala la mtoto. Sina maana najua aliyemteka, ila naweza kukusaidia jinsi gani ya kufanya ili tujue mtoto yuko wapi."

"Mmmmh, basi kesho asubuhi."

"Lakini naomba jamaa asijue lolote. Tukutane mimi na wewe tu sawa?"

"Sawa Jerry, kama ni kweli, nitashukuru sana."

**Ilikuwa rahisi kwa mwanamume kupishana naye akashindwa kugeuka. Iwe akikutana naye kwa mbele na lazima atageuka akishapitana naye, na hata kama atakuwa nyuma yake, akishampita tu atagauka kuangalia sura.**



"Sasa ungehitaji tukutane wapi?" Jerry aliuliza. Alichotaka ni kumpa uhuru bibie achague sehemu ambayo atahisi haitokuwa hatari kwake, au kutokuwa na wasiwasi kwa ni yeye ni mke wa mtu.

"Wewe ndiyo mwenye hiyo habari, sasa wewe panga tukutane wapi?"

"Hapo jamaa utamuagaje sasa?"

"Huyu niachie mimi. Naweza kumwambia naitwa kwanza kazini, kwa sababu tangu tukio hili litokee wiki nzima sijaenda kazini."

"Okay, vizuri kesho basi Neema, pole sana."

"Nishapoa Jerry."

**********************************

Neema alishuka kwenye bodaboda maeneo ya Karume, Ilala jijini Dar es Salaam. Ndipo alipoahidiana na Jerry. Alivuka barabara. Kwa mbali aliliona gari la Jerry. Alilifahamu vyema. Alitembea taratibu hadi akalifikia. Tayari Jerry alikuwa ameshafungua kitufe cha kuuloki mlango.

Haraka Neema alifungua mlango na kuingia.

Ni kitendo bila kuchelewa, gari liliondoka kwa kasi. Nusu dakika ya kimya. Jerry alianza kumsalimia. "Za siku nyingi Neema."

"Si nzuri sana Jerry, kama unavyojua. Mtoto wangu ameporwa. Hapa unaponiona sina moja wala mbili, hata sielewi nifanye nini."

"Pole sana, hata mimi imenioma sana. Unajua wewe Neema ni rafiki yangu, kwa hiyo nimeona ni lazima nami nitoe mchango wangu mdogo tu wa kukusaidia."

"Kwani una tetesi zozote au?"

"Subiri kwanza Neema. Hili suala ni zito. Inabidi twende sehemu tukae nianze kukupa moja baada ya lingine. Halafu nadhani baada ya hapo, wewe na mimi tujue nini tunafanya, sawa?"

"Sawa." Alijibu kwa sauti ya unyonge.

"Tunakwenda wapi sasa? Grosari au hotelini kwa ajili ya kulizungumzia hili?" Jerry aliuliza, lakini tayari mwenyewe akiwa na jibu moyoni.

"Mimi nadhani wewe ndiye unaweza kuona wapi twende."

"Sikiliza Neema. Hili ninalotaka kukwambia ni suala nyeti ambalo hapaswi asikie mtu yoyote au hata adhani tu hawa wanazungumzia nini. Linatakiwa kuzungumzwe sehemu ambayo tuko mimi na wewe tu."

Kwenye akili ya Neema yeye hakuwa anawaza chochote kile kuhusu mahali pa kuzungumzia. Alichokuwa anawaza ni kitu gani kimempata mwanawe. Hata angeambiwa waende kwenye sayari nyingine ukiondoa dunia, alikuwa tayari kwa wakati huo.

Alimtazama Jerry kwa jicho ambalo lilizungumza na kumuuliza ni wapi waende kuzungumzia.

"Mimi nadhani nyumbani kwangu kunafaa sana." Macho ya Neema yalibadilika. Jinsi alivyomtazama mwanzo ilikuwa ni tofauti sasa na utazamaji huu wa sasa.

Ulionekana ni kama utazamaji wa mshangao.

"Huna mke huko nyumbani au mpenzi?" Aliuliza kwa hali ilionekana kama mzaha, lakini ujumbe ulifika kwa mlengwa.

"Siku nyingi nilikwambia sina mke, sijaona na ndiyo maana nilikwambia kuwa nilitaka kukuoa wewe, lakini kwa bahati mbaya nimekukuta umeshaolewa, basi tena."

"Mmmmh, ina maana baada ya kunikosa mimi hutooa tena we Jerry?"

"Sijajua. Ni hapo itakapokuja yenyewe. Mbona nilikuwa sijaona na nilikuwa sina wazo hilo, lakini nilipokutana na wewe wazo la kuoa likanijia. Kwa hiyo pindi mwaka, nikikutana na mwanamke ambaye atatokea kumpenda kama nilivyokupenda wewe, basi nitamuoa."

Ilikuwa sauti iliyoonyesha jinsi gani Jerry alikuwa anaumia kwa kumkosa Neema. Mwanamke aliyetokea kumpenda, lakini alikutana naye akiwa tayari ana ndoa ya miaka mitatu sasa.

Tayari walikuwa wamefika maeneo ya Chang'ombe Maduka Mawili ambako Jerry alikuwa anaishi. Kutoka Chang'ombe hadi Keko hakukuwa mbali sana. Lakini Neema alichukua bodaboda hadi Karume na Jerry aliondoka nyumbani kwenda kumsubiria Ilala kwa ajili ya kupoteza lengo kama kuna mtu alikuwa akimfuatilia Neema.

Kwa haraka haraka kama mwanamke, Neema alitupa macho kila kona ya sebule kuangalia kama ni mazingira ambayo mwanamke mwenzake anaishi. Dakika mbili baadaye akawa na uhakika kuwa ni sehemu ambayo hajakanyaga mwanamke yoyote kwa zaidi ya mwezi mmoja au miwili hivi.

Kilichofuatia ni Jerry kumweleza hatua moja baada ya nyingine jinsi ilivyotokea tangu alipomwona na mumewe wakivuka barabara hadi kituoni. Alivyoporwa mtoto na yeye kuchukua bodaboda na kulifuatilia gari hilo hadi maeneo ya Ubungo Maziwa lilizama kwenye geti la jumba moja la kifahari.

Kwa ushahidi, Jerry alionyesha picha ya gari ambalo mtekaji aliondoka nalo, alipolipiga kwa kutumia simu yake na mkononi siku ile. Neema aliangua kilio. Kilio kikichofuatia kumkumbatia kwa nguvu Jerry.

"Jerry nisaidie Jerry, sasa tutafanyaje ili mimi nimpate mtoto wangu Diana..."

"Kwa mbali Jerry alihisi msisimko wa faraja. Kukumbatiwa na mwanamke anayempenda lilikuwa jambo la furaha sana. Lakini kwa wakati huo mwanamke hakuwa na furaha. Hivyo naye hakutaka kuusikilizia sana msisimko alioupata.

"Usilie mama. Ndiyo maana nimekuita hapa ili tujue nini tunafanya mimi na wewe ili kumuokoa mtoto kwenye mikono ya mtekaji sawa?"

"Kumbe kweli Jerry nimeamini unanipenda. Yaani umeamua kumfutilia mtekaji hadi alikoishia kwa ajili yangu?" Aliongea Neema kwa sauti ndogo, akiwa hajui kama anamuuliza Jerry au anamjibu.

"Hilo halina maana kwa sasa. Kikubwa hapa ni kutafuta mbinu za kumpata Diana wako." Alisema na kunyamaza huku bado akiwa ameegemewa na Neema.

"Kwa sasa ninachoomba siri hii iwe kwetu sisi wawili tu kuwa mtoto alipelekwa wapi. Mumeo asijue na wala kwa sasa tusiripoti polisi kwa sababu chochote tutakachofanya haraka haraka tunakosa mwana na maji ya moto. Hatujui mtoto yuko kwenye hali gani. Tunachotakiwa tujue kwanza mtoto bado yumo mle ndani? Yupo hai? Yupo na nani? Nadhani baada ya hapo huko mbele tutajua cha kufanya sawa?"

"Mimi nakusikiliza wewe tu Jerry. Nitafuatisha vile utakavyoniambia. Mradi tu mtoto wangu apatikane."

**INAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# LUPITA AMKEJELI WAZIRI WAKE

MWIGIZAJI wa filamu za Hollywood mwenye asili ya Kenya, Lupita Nyong'o, amemjibu Waziri wa Utalii wa nchini humo, Najib Balala, kuwa anashangazwa na kauli yake ya kumtafuta kwa miaka mitano.

Lupita ameandika katika ukurasa wake wa Twitter, kwamba wakati anatafutwa na serikali ya Kenya, labda yeye alikuwa katika nchi ya kufirika ya Okanda ambayo imeigizwa katika filamu ya Black Panther.

Wakenya wamekuja juu baada ya nafasi hiyo kupewa mwanamitindo maarufu Naomi Campbell wa Uingereza.

## Dicky Flavour azidi kupaa

MSANII anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Dicky Flavour, amewashukuru mashabiki wake kwa kuipokea vizuri ngoma yake 'Tuyamalize' ambayo inazidi kutesa.

Dicky Flavour, amesema tangu aachie wimbo wake huo ameungwa mkono na wadau wote wa muziki kuukubali na kusababisha idadi ya watu wanaotazama kupitia You Tube kuongezeka kila siku.

"Namshukuru Mungu kwa jinsi anavyonitendea katika kazi yangu, tangu nitambulishe wimbo wangu mpya, mashabiki wameupokea vizuri na naona faraja kuona idadi kubwa wananiunga mkono," amesema Dicky Flavour.



## Harmonize kwa hili Mungu atakubariki

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Harmonize, ametoboa siri kwamba wimbo wake wa kwanza 2021 amemshirikisha Anjella, ambaye licha ya kuwa chipukizi lakini amefanya maajabu.

Katika ukurasa wake wa Istagram, Harmonize amekiri kuwa amesema na moyo wake na kuona hawezi kumuacha kutokana na binti huyo kuwa na kipaji cha kipekee katika muziki.

"Niliumbia moyo wangu kwamba siwezi kuona kipaji cha huyu dada kinateketea eti kwasababu tu ana ulemavu ambao amebarikiwa na Mungu ambae kazi yake haina makosa. Liwe kwenye jua au mvua nitahakikisha kipaji chake kinawafikia , mtaamua nyinyi kumuunga mkono au laa,"Sehemu ya ujumbe huo inasema.



HABARI MICHEZO

# Mbappe afikiria mkataba mpya PSG

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema anafikiria kusaini mkataba wa muda mrefu na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, klabu ya Paris Saint-Germain.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alimaliza ukame wa kutofunga kwenye mechi nne juzi Ijumaa, wakati alipotikisa nyavu mara mbili na kutoa pasi moja ya mwisho kwa kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino kilichoibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Montpellier.

Majaliwa ya Mfaransa huyo yameonekana kuwa shakani hivi karibuni na hakuwa kwenye kiwango, huku mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika msimu ujao.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Leonardo alithibitisha kupitia jarida la France Football wiki hii kwamba anajiamini, Mbappe na mchezaji mwenzake, Neymar wataongeza mikataba ya kukaa pale Parc des Princes.

Mbappe, ambaye alihusishwa na klabu kama Real Madrid na Liverpool, amesema anaweza kusaini mkataba mpya.

"Tunazungumza na klabu," alisema akiiambia Telefoot. "Pia naangalia hilo. Kama nitasaini, itakuwa ni uwekezaji wangu mwenyewe wa muda mrefu hapa."

"Najisikia vizuri hapa. Haraka hivi karibuni nitafanya uamuzi. Kama nitaongeza, maana yake nitabaki."






# ARTETA AIBUKA AKIMTETEA LAMPARD

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ana matumaini Frank Lampard atapewa muda zaidi pale Chelsea wakati kocha huyo akikabiliwa na matokea mabaya kwenye Ligi Kuu England.

Chelsea walipaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakati walipoibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Leeds United Desemba 5, mwaka jana lakini imechukua pointi saba tu katika mechi nane zilizopita.

Matokeo ya mechi hizo nane yanajumuisha kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa kikosi cha Arteta, Arsenal walipokutana Desemba 26, mwaka jana, matokeo ambao yalimaliza ukame wa washika bunduki hao kutoshinda mechi saba mfululizo.

Na sasa Arteta ameamua kumtetea kocha mwenzake huyo kwamba, anatakiwa kuendelea kuaminiwa pale Stamford Bridge.

"Nimemjua Frank kwa miaka michache na kuna wakati tumekuwa pamoja," alisema Arteta akiviambia vyombo vya habari.

"Ningependa (Chelsea) impe sapoti na nafasi. Ana uzoefu mkubwa kama mchezaji, ni nembo pale.

"Amefanya mambo mengi mazuri, lakini unahitaji muda kama kuna vitu haviendi sawa, na uvumilivu ndio jambo muhimu zaidi."

Arteta, ambaye naye nafasi yake ilikuwa shakani wakati Arsenal ikiwa na matokeo mabaya mwanzoni mwa msimu huu, anahisi klabu zitanufaika kama zikionyesha uvumilivu.

# *Kevin De Bryune nje kwa wiki sita*

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bryune, atakosekana kwenye kikosi cha timu hiyo kwa takribani wiki nne hadi sita, hii ni baada ya kupata majeruhi.

De Bryune aliumia kwenye mchezo dhidi ya Aston Villa siku ya Jumatano na atakosa takribani mechi 10 zikiwamo za Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola amethibitisha kukosekana kwa De Bryun akisema; "baada ya uchunguzi, daktari amesema Kevin atakuwa nje kati ya wiki nne hadi sita."

"Ni habari mbaya kwetu, lakini tunapaswa kusonga mbele."

City hawajapoteza mchezo katika mechi 16 walizocheza kwenye mashindano yote na sasa wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England nyuma ya vinara, Manchester United.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAKARIBIA KUMNASA ODEGAARD

●●● Kocha Arteta afunguka mazungumzo ya kunasa saini ya kiungo huyo yako...

**LONDON,** England

ARSENAL wana matumaini ya kumsajili kiungo, Martin Odegaard kwa mkopo katika siku zijazo akitokea kwa vigogo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid.

Mazungumzo yanaendelea na Real Madrid juu ya makubaliano ya kiungo huyo mshambuliaji na wanaweza kumpata mchezaji huyo hadi mwisho wa msimu huu.

Ilionekana kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway angerejea kwa msimu mwingine kwa mkopo kutoka Real Sociedad, baada ya kuwa mwaka mzuri aliotumia kule San Sebastian wakati wa msimu wa 2019-20.

**Lakini Arsenal sasa wamekuja mstari wa mbele kumwania Odegaard, ambaye aliomba ruhusa ya kuondoka Real Madrid mwezi huu ili kupata muda zaidi wa kucheza.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye anaweza kucheza kama namba 10 au winga ya kulia, amecheza mechi tisa tu kwa mabingwa hao wa Hispania msimu huu.

"Tuko katika mchakato huo hivi sasa," alisema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akiwaambia waandishi wa habari juu ya taarifa ya mchezaji huyo.

"Tumefanya sehemu ya kwanza (kupunguza kikosi), zaidi au chini, na sasa tunazingatia awamu ya pili.

"Ni wazi soko hili na muktadha hufanya iwe ngumu sana, lakini tunaangalia uchaguzi na tutaona ni nini tunaweza kufanya."

## ZISIKUPITE

### RICE RASMI SOKONI

KIUNGO wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, anaweza kupatikana kwa pauni milioni 50 kipindi cha majira ya joto na hapo inawezekana Chelsea, Liverpool, Manchester City na Manchester United zikamwania. ***(90 Min)***

### VIRGIL MAMBO SAFI

LIVERPOOL imeamua kuupa kipaumbele mkataba mpya wa mlinzi wake wa kati, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 29, kabla ya kufikiria mazungumzo ya mkataba mpya na fowadi wa Misri, Mohamed Salah ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Eurosport)***

### POGBA NJIA PANDA

KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba (27), atachelewa kuchukua uamuzi juu ya majaliwa yake hadi mwishoni mwa msimu huu, wakati klabu hiyo ya Old Trafford ikitoa changamoto ya kuwania taji la Ligi Kuu England msimu huu. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMTAKA BERTRAND

ARSENAL inafikiria kumsajili mlinzi wa kushoto wa Southampton na England, Ryan Bertrand (31), ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja, wakati wakiangalia kuleta ushindani kwa mlinzi wa Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 23. ***(Evening Standard)***

### VARANE KUONDOKA MADRID

MLINZI wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 27, anataka kuondoka Real Madrid. ***(Sport)***

### MOURINHO AMKANA INGS

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amekanusha uvumi kwamba anataka kumsajili straika wa Southampton na Timu ya Taifa ya England, Danny Ings (28). ***(Express)***

### EDOUARD KUMRITHI VARDY

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, anafikiria kumsajili Osdonne Edouard mwenye umri wa miaka 23 kama mrithi wa muda mrefu wa straika, Jamie Vardy. ***(Talksport)***

### BENTEKE KUTUA BROM

KLABU ya Crystal Palace ipo tayari kumuuza straika, Christian Benteke, huku West Brom ikionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Mail)***

### BRUCE AMTAKA JONES

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce, amesema anahitaji kumwongeza kocha wa Bournemouth, Graeme Jones katika orodha ya wasaidizi wake. ***(Sun)***

### MOYES KITAELEWEKA

KLABU ya West Ham inapanga kumpa ofa ya mkataba mpya, David Moyes mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

HABARI MICHEZO

## Makamu wa Rais ZFF atimuliwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Salum Ubwa, ameondolewa madarakani baada ya kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye na wajumbe wa mkutano mkuu wa shirikisho hilo waliokutana Visiwani hapa jana.

Ubwa aliondolewa madarakani baada ya kupigiwa kura 14 huku wengine 11 wakitaka aendelee na nafasi yake katika mkutano huo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Kilimani.

Wajumbe 21 wa mkutano huo pia walimpigia kura za kuwa na imani na Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu huku kura nne zikimkataa huku pia wakionyesha kumkubali Mjumbe wa Kamati Utendaji aliyeteuliwa na Rais wa shirikisho hilo, Ali Mohammed Ameir.

Mkutano huo pia uliridhia Mwenyekiti wa Soka la Wanawake Zanzibar, Nasra Juma, aendelee na nafasi yake kama kawaida kwa kupata kura 20 huku Ali Mohamed ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano alipata kura 23, hivyo ataendelea kulitumikia shirikisho hilo.

Wajumbe wa mkutano huo walifikia ajenda hiyo baada ya kutokuwa na imani na viongozi hao wa juu pamoja na Kamati ya Utendaji kutokana na kugubikwa na 'mizozo' ya mara kwa mara ndani ya shirikisho hilo.

Wajumbe wengine wa Kamati ya Utendaji waliobaki madarakani ni Haji Hassan kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi ambaye alipata kura 20 huku Seif Bausi kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja alitangaza kujiuzulu kabla ya zoezi la kupigiwa kura halijaanza.

## Coastal Union yaitaka Simba

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umeandika barua kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wakitaka kucheza nao mechi ya kirafiki kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mechi za mzunguko wa pili wa ligi hiyo utakaoendelea mapema mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Coastal Uinion, Rashid Mgweno, alisema baada ya kuongeza nguvu katika usajili wa dirisha dogo wanahitaji mechi mbili za kirafiki na kuzitaja timu walizoomba ni Simba na Polisi Tanzania.

Mgweno alisema wanasubiri majibu kutoka kwa viongozi wa timu hizo na endapo maombi yao yatakubaliwa, wanaimani zitawasaidia kwenye maandalizi ya duru la lala salama.

Alisema wakati huu ligi imesima, wao wameendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiweka sawa kwa sababu ya kukosa maandalizi mazuri wakati msimu huu ulipoanza kutokana na changamoto mbalimbali za wakati huo.

Aliwataja wachezaji waliosajiliwa ili kuongeza nguvu katika kikosi chao ni pamoja na beki wa kati, Ally Ally, Pascal Kitenge kutoka DRC na mshambuliaji, Francis Mustapha wa Burundi.

# KUMEKUCHA TIGO KILI HALF MARATHON 2021

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MBIO maarufu za Tigo Kilimanjaro Half Marathon (2021), zimezinduliwa rasmi kimkoa kwenye viwanja vya Kibo Palace Homes, mjini hapa kwa kushirikisha wadhamini, viongozi wa Chama Cha Riadha Mkoa wa Kilimanjaro (KAAA), wadau wa mchezo huo na waandaaji.

**Akizindua mbio hizo, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Alhaj Rajab Kundya, aliwapongeza wadhamini na waandaaji wakiongozwa na kinywaji cha bia ya Kilimanjaro kwa kazi nzuri wanayoifanya na kusema wamezifanya mbio hizo ziwe maarufu zaidi.**

Kundya alisema mbio hizo zimeendelea kuutagaza Mkoa wa Kilimanjaro na kuipongeza Kampuni ya Tigo kwa kutoa hamasa kwa Watanzania katika masuala ya kijamii hasa michezo.

"Hii iwe changamoto kuwafanya Watanzania wakimbie kwa kasi zaidi ili washinde hata zawadi nyingine kubwa zinazotolewa na waandaaji," alisema Kundya.

Kiongozi huyo pia alitoa wito kwa wafanyabiashara kutumia fursa hii vizuri kwa kufanya biashara tofauti tofauti wakati wote kuelekea siku ya mbio hizo.

Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo alisema: "Tigo tunajivunia kuwa wadhamini wakuu wa mbio maarufu za Tigo Kili Half Marathon kwa mwaka wa sita mfululizo. Tukiongoza sokoni kwenye mageuzi ya maisha ya kidijitali yakiwamo masuala ya fedha, tunafurahi kwa mara nyingine tena kuwezesha usajili na malipo kwa washiriki kwenye mashindano hayo yajayo kupitia kwa huduma zetu kamilifu za fedha Tigo Pesa,".

Kinabo alisema kwa muda mrefu Tigo Pesa imethibitisha kuwa bora zaidi na mfumo wa kuaminika wa malipo kwa wanariadha wote wenye nia ya kushiriki kutoka sehemu yoyote hapa nchini.

"Zaidi ya hapo, tunamkaribisha kila mmoja kwa ajili ya kupata kumbukumbu za mashindano hayo na kutumia wengine kupitia mtandao wenye kasi zaidi Tanzania wa 4G+," Kinabo alisema.

Aliongeza hadi kufikia juzi zaidi ya wanariadha 4,039 wamejiandikisha na watakaokimbia mbio za Killi Marathon ni watu 310 na kwa upande wa Tigo Kili Half Marathon ni 3,469 huku Fun Run ambayo watakimbia umbali wa kilomita tano ni washiriki 260 .

"Tumeandaa Sh. milioni 12.5 kwa ajili ya washindi 10 wa kwanza upande wa wanaume na wanawake," alisema.

Meneja Chapa wa TBL, Irene Mutiganzi alisema Kilimanjaro Premium Lager inajivunia kudhamini mbio hizo kwa miaka 19 sasa kutokana na weledi na uzoefu mkubwa wa waandaaji ambao wamefanya mbio hizo ziwe maarufu na moja ya matokeo makubwa nchini huku akiitaja kauli mbiu ya mwaka huu ni 'Twenzetu Kili'.




Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa mbio za Tigo Kili Half Marathon uliofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Azam yazialika Express, Dynamos

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Simba ikizialika timu za TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na Al Hilal ya Sudan kwenye mashindano maalumu ya Simba Super Cup, Azam FC nayo inazileta nchini Lusaka Dynamos ya Zambia na Express kutoka Uganda kwa ajili ya mechi za kirafiki ili Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema baada ya kucheza mechi za Kombe la Mapinduzi huko Zanzibar na mchezo mwingine wa kirafiki hapa jijini Dar es Salaam, sasa kikosi chao kitacheza mechi za kirafiki za kimataifa ili kuendelea kuangalia upungufu wao kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu Bara.

Zacharia alisema uamuzi wa kuzialika timu hizo umetokana na maombi ya Kocha Mkuu, George Lwandamina ambaye alihitaji kuiongezea nguvu timu yake ambayo ilitolewa hatua ya nusu fainali kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati amesema mechi hizo mbili za kirafiki watakazocheza zitawasaidia kuboresha upungufu wa kikosi chao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Vivier alisema kambi ya siku 10 waliyokaa Zanzibar imewasaidia kujenga timu kwenye kila idara na tathimini inaonyesha mazoezi waliyofanya yameimarisha viwango vya wachezaji baada ya kuona mabadiliko.

"Tumerudi nyumbani na kutafuta mechi mbili na timu kutoka nje kwa ajili ya kufikia mahitaji yetu yote kwa asilimia 100%, baada ya kubaini upungufu tulipokuwa Zanzibar," alisema Bahati Vivier.

# Michezo

Jumapili Januari 24, 2021

Nipashe





Arsenal yakaribia kumnasa Odegaard UKURASA 22




Kiungo wa Timu ya Taifa ya Rwanda, Kalissa Richard (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Morocco, katika mechi ya Kundi C ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), iliyochezwa juzi usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

## Karia azipasha klabu Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, amesema bado kuna matatizo katika suala la uendeshaji na utawala bora kwenye ngazi ya klabu.

Karia alisema hayo wakati wa ufunguzi wa semina ya Mafunzo ya Utawala Bora iliyowashirikisha wenyeviti wa klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilifanyika jana visiwani hapa.

Rais huyo alisema kwa sasa TFF imefanikiwa kufanya kazi kwa weledi na viongozi wa mikoa ambayo ni wanachama wa shirikisho hilo lakini kwa upande wa klabu bado ni tatizo.

Alisema ili shughuli za klabu zifanyike vyema, ni lazima kuwapo kwa mgawanyiko wa majukumu na sio kila kazi ifanywe na mtu mmoja.

"Utakuta katika klabu kuna mtu mmoja ambaye yeye ndiye anayefanya majukumu yote huku akisahau kuwa kila kiongozi anatakiwa atekeleze majukumu yake. Haiwezekani, hatutaki kuona mtu mmoja huyo ndiye anakuwa anatekeleza kila kitu ni lazima tuwe na mgawanyo wa madaraka," alisema Karia.

Aliongeza licha ya kutoa mafunzo mbalimbali, bado tatizo hilo halijamalizika kwa sababu viongozi wanaohudhuria semina hizo ni wale wale ambao wamechaguliwa kushika nafasi za uongozi.

Kiongozi huyo alishukuru kuona mafunzo ya jana yaliwashirikisha wahusika halisi na anaamini watakaporejea Tanzania Bara watakuwa wamepata elimu itakayowasaidia katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Utawala Bora.

Naye Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Salum Ubwa, aliwaomba viongozi wa TFF kuendelea kuwasimamia vyema ili na shirikisho lao lifikie malengo yake kama ambavyo Tanzania Bara inavyojiendesha.

"Tunataka kuiona Zanzibar inakuwa na shirikisho kubwa lakini tunashindwa kufikia hapo tunapopahitaji, jambo ambalo tunaomba kusaidiwa," alisema Ubwa.

Semina hiyo elekezi inayosimamiwa na TFF inatarajiwa kuendelea tena leo kwa kushirikisha viongozi wa klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar.

# Simba yashusha kocha mkufunzi

## ●●● Lengo ni kukamilisha hesabu zake, kutambulishwa Jumatatu katika...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kikitarajiwa kuanza rasmi mazoezi hapo kesho, mabosi wa klabu hiyo wamesema watahakikisha wanaajiri kocha mpya ambaye atahakikisha klabu hiyo inafikia malengo yake yote iliyojiwekea.

**Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa juu wa Simba (jina tunalihifadhi), alisema klabu iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato huo na makocha wote watatu walioingia kwenye mchujo wa mwisho wana viwango vya juu.**

Kiongozi huyo ambaye alikataa kuweka wazi majina ya makocha hao, alisema wamejipanga kuleta mapinduzi ya soka hapa nchini na hii imetokana na kujifunza kupitia vigogo wengine wa Afrika ambao wamewahi kupata mafanikio ya juu.

"Tuko kwenye kikao (jana), lakini kwa kifupi timu itaanza mazoezi Jumatatu na tayari mtakuwa mmefahamu kocha mpya ambaye ataiongoza Simba, safari hii tumepanga kuja tofauti," alisema kiongozi huyo ambaye pia ni mtendaji.

Aliongeza wamedhamiria kufanya vizuri zaidi msimu huu kwa kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na vile vile kuishangaza Afrika kwa kufika fainali au kubeba taji hilo kwa mara ya kwanza.

"Kikwazo kitakuwa ni kufika robo fainali, kama hapo tutavuka, ujue hakuna ambaye atatushika huko mbele, kasi yetu hawataiamini, tumeshiriki kwa muda mrefu mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tumejifunza vitu vingi, sasa tunaenda kwa mikakati zaidi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kwa sasa Simba haina tatizo la fedha na suala la kukamilisha mchakato kumpata kocha linaendeshwa kwa weledi kwa sababu wanataka kuweka historia nyingine ya juu chini ya utawala wa Rais, John Magufuli.

"Kocha atakayekuja atakuwa anajua malengo ya Simba, kiu tulichonacho Simba, pia ni suala la kuzingatia hesabu, kumbuka mwaka juzi tulifungwa mabao 5-0 ugenini mara tatu, lakini sisi tuliangalia zaidi pointi na zilituvusha," kiliongeza chanzo chetu.

Wakati huo huo, viingilio kwa ajili ya mashindano ya Simba Super Cup vimetangazwa cha juu kwa upande wa VIP A kikiwa ni Sh. 25,000, VIP B na C Sh. 15,000 na mashabiki watakaokaa eneo la mzunguko watalipia Sh. 3,000.

Mechi ya ufunguzi ya mashindano hayo yaliyoandaliwa kwa ajili ya kuziandaa timu shiriki na mechi za hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itacheza Januari 27, mwaka huu kati ya Simba dhidi ya Al Hilal na itafuatiwa Januari 29, mwaka huu kwa Wasudan hao kukutana na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Januari 31, mwaka huu utachezwa mchezo wa mwisho kati ya wenyeji Simba dhidi ya TP Mazembe na bingwa wa michuano hiyo atapewa kikombe maalumu.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042